# Nipashe

Jumatano Novemba 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581852

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


UKURASA WA 4

**Mbunge** ashtuka idadi ya watoto wanaolala kwenye mabaraza maduka



UKURASA WA 4

**Hata** tukibaki na mgombea mmoja, hatujitoi Uchaguzi Mitaa - CHADEMA





UKURASA WA 19

**Ni** mtifuano wa Kamala, Trump kusaka kiti cha Ikulu Marekani

## WIZARA YA AFYA:

# Kasi maradhi ya figo yachochewa na haya

UKURASA 2



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel

## Waziri atuma timu kuchunguza kashfa kampuni ya madini

UKURASA 3

## Kanisa Anglikana lang'aka jina lake kutumika vibaya

UK. 2





Skani hapa kutembelea chaneli yetu


**MICHEZO** SIMBA YAPANIA KUKAA KILELENI LEO UK.24

**MAONI,** UK.6



Mkurugenzi wa Kampuni ya Vanilla International Ltd, Saimon Mnkondya, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, huku amefunika uso, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka 28 yakiwamo ya kuendesha biashara ya upatu, utakatishaji fedha, uhujumu uchumi na kujipatia viwanja mbalimbali. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wizara: Mambo manne yachangia ongezeko wagonjwa wa figo nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imetaja sababu nne zinazochangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la wagonjwa wa figo nchini kuwa ni pamoja na matumizi holela ya dawa za maumivu.

Naibu Waziri, Dk. Godwin Mollel aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Sylvia Sigula ambaye alitaka kujua chanzo cha ongezeko la wagonjwa wa figo nchini.

Dk. Mollel alisema ongezeko hilo pia linachangiwa zaidi na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, hususani shinikizo la damu na kisukari.

Alitaja sababu nyingine ni matumizi holela ya dawa, hasa za maumivu, watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) wasiokuwa na ufuasi mzuri wa dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo na kutozingatia mtindo wa maisha unaofaa hususani matumizi makubwa ya chumvi, tabia bwete na matumizi ya vilevi, hasa pombe na bidhaa za tumbaku.

Naibu Waziri Mollel alisema serikali inaendelea kutoa elimu na kuasa jamii kuhusu kujikinga kwa kubadili mtindo wa maisha, ambao unajumuisha ulaji usiofaa hususani matumizi makubwa ya chumvi, vyakula vyenye sukari nyingi au nafaka zilizokobolewa.

Alisema serikali imeimarisha huduma za matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza pamoja na matibabu ya VVU/Ukimwi ili kuzuia madhara ya magonjwa hayo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Jacquline Kainja, alihoji mpango wa serikali kudhibiti matumizi holela ya dawa za binadamu ambazo zimeonekana kuwa moja ya sababu zinazochangia maradhi ya figo.

"Nini mpango wa serikali kuwezesha hospitali zake kutoa huduma ya kusafisha figo na kuwaondolea adha wagonjwa kwenye upatikanaji huduma na gharama za matibabu?"mbunge huyo alihoji.

Naibu Waziri Mollel, akijibu maswali hayo, alisema serikali inaendelea kuelimisha jamii kuhakikisha matumizi ya dawa yanazingatia maelezo ya daktari na mtu anapokwenda kununua dawa kwenye duka la dawa, awe ameandikiwa na daktari.

Hata hivyo, alisema katika kupunguzia wananchi mzigo wa matibabu ni suala la bima ya afya kwa wote na serikali inaimarisha upatikanaji vifaa tiba na dawa kwa kununua moja kwa moja viwandani badala ya kununua kwa watu wa kawaida.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Cecilia Pareso alisema gharama za kusafisha figo katika hospitali binafsi na za serikali zina utofauti wa bei.

"Ukienda kusafisha figo hospitali za binafsi ni nafuu kushinda hospitali za serikali, ni ghali! Nini mkakati wa serikali kupunguza gharama hizi ili wagonjwa wapate unafuu na matibabu?" alihoji.

Dk. Mollel, akijibu swali hilo, alisema hospitali za serikali zinatakiwa kuwa na gharama nafuu na kuahidi kulifuatilia suala hilo.

Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Kunti Majala alihoji kama serikali iko tayari kupunguza gharama za usafishaji figo kutoka Sh. 300,000 hadi Sh. 50,000 kutokana na mchakato wa bima ya afya kwa wote kusuasua.

Naibu Waziri Mollel, akijibu swali hilo, alisema kuna uzinduzi mkubwa wa mpango huo wa bima ya afya kwa wote umefanyika jijini Arusha hivi karibuni na ni kiashiria cha kuanza kutekelezwa kwa suala hilo ili watanzania wawe na uhakika wa matibabu.

Alisema kuna timu inafanya kazi kuhakikisha gharama hizo zinapungua.

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# Kanisa Anglikana latoa tamko matumizi mabaya jina lake

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

KANISA la Anglikana Tanzania limeomba serikali kupitia Msajili wa Jumuiya na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kuchukua hatua stahiki za kusitisha matumizi ya majina ya makanisa ambayo yanaiga yale yaliyokwishasajiliwa.

Ombi hilo linakuja huku kukidaiwa kuwa kumekuwapo na mpasuko mkubwa ndani ya kanisa hilo baada ya mchungaji mmoja kujiondoa na kuanzisha kanisa jipya ambalo limeondoka na makanisa saba ndani ya Dayosisi ya Mpwapwa.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Mchungaji Canon Bethuel Mlula, alitoa ombi hilo jana jijini hapa, wakati akisoma tamko kwa vyombo vya habari kuhusu kuanzishwa kwa kanisa jipya la Episcopal Anglican Province of Tanzania.

"Serikali kupitia Msajili wa Jumuiya na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunaomba kuchukua hatua stahiki za kusitisha matumizi ya majina ya makanisa ambayo yanaiga makanisa yaliyokwisha sajiliwa ikiwamo Kanisa la Free Anglican Church of Tanzania, Kanisa la Kiinjili la Aglikana na Episcopal Anglican Province of Tanzania," alisema Canon Mlula.

Alisema serikali inapaswa kuzuia madhehebu ya dini matumizi ya majina yanayofanana jambo ambalo sio tu linaleta mkanganyiko, bali pia linafanywa kwa makusudi, ili kuwawezesha wale wanaoanzisha kujificha humo kupata waumini na kuwafanya mateka wa kiroho.

"Aidha, kutokana na uzoefu wa hivi karibuni wa baadhi ya makanisa yanayoanzishwa na wageni kutumia kudanganya Watanzania, tunaiomba Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kufanya uhakiki wa kina madhehebu ya dini na wamiliki wake kabla ya kuamua kuyaruhusu kufanya huduma zake hapa nchini," alisisitiza.

Aidha, alisema kwa kutambua haki ya kikatiba ya kila Mtanzania kuabudu pasipo kuvunja sheria wanaiomba serikali kulitazama kwa makini sana jambo hilo na kuchukua hatua stahili.

"Serikali ichukue hatua stahili za kuwakamata wamilikii wa Kanisa hili la Episcopal Anglican Church of Tanzania na makanisa mapya yenye kushabihiana na yale yaliyopo toka zamani kubadili mara moja majina yao pia kuzingatia sheria na taratibu za nchi katika kujiendesha," alisema.

Kadhalika, alisema viongozi wa dini wanatoa rai kwa serikali kuweka mifumo madhubuti ya kuratibu haki za uanzishwaji wa jumuiya za kidini kwa nia njema ya kulinda amani, umoja na mshikamano wa Watanzania.

"Serikali itazame upya pia usajili wa makanisa ambayo yanashabihiana majina kwa kuwa baadhi ya viongozi wake wanatumia mbinu hiyo, ili kuwavuruga na kuwapotosha waumini na hatimaye kuwafanya watumwa wa imani," alisema.

Vile vile, alisema kanisa linawajulisha waumini wote kubaki watulivu ndani ya kanisa lao wakati taratibu za ndani za kushughulikia suala hilo zinaendelea.

"Ijulikane pia kwamba kanisa la Episcopal Anglican Province of Tanzania kamwe si sehemu ya Kanisa Aglikana Tanzania wala Kanisa Aglikana Duniani," alisema Canon Mulula.

Pia, alisema shutuma za masuala ya ushoga ambazo zinatolewa dhidi ya Kanisa Aglikana Tanzania na baadhi ya viongozi wanaoasi na kuanzisha makanisa mengine ni hoja ya kutaka kuichafua sifa ya kanisa.

"Kanisa Anglikana Tanzania halijawahi kuunga mkono masuala ya ushoga na hayo mambo ambayo yanaelezwa na baadhi ya wachungaji ambao wamekimbia na kuanzisha madhehebu yao ni hoja za kulichafua kanisa," alisema Canon Mlula.

HABARI KITAIFA

# Utekelezaji mradi wa EACOP wanufaisha Watanzania 7,500

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTEKELEZAJI mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga umefikia asilimia 45.5 huku Watanzania 7,584 wakinufaika na fursa ya ajira.

Akizungumza jana jijini hapa wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa mkoa wa Dodoma kuhusu utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati wa serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mratibu wa Mradi huo, Asiadi Mrutu, alisema kuwa hadi kufikia Septemba mwaka huu, Watanzania hao walinufaika na fursa hiyo ya ajira.

Alisema kwa kipindi hicho serikali imeingiza Sh. bilioni 10.69, ikiwa ni pango la ardhi ya mradi na kwa sasa maandalizi ya kulaza bomba ardhini yanaendelea.

"TPDC kwa kushirikiana na EACOP imetekeleza zoezi la uhamishaji makaburi kwenye eneo la Mkuza ambapo hadi sasa makaburi 1,146 yamehamishwa na huu uhamishaji makaburi umekuwa shirikishi na unaozingatia taratibu za nchi na za kimataifa," alisema.

Alisema kwa kila kaburi, kiasi cha Sh. 300,000 kililipwa kama rambirambi ili kuhamishwa.

"Zoezi la kuhamisha makaburi lilikuwa shirikishi na kushirikiana na familia na mradi uliheshimu sana hizo taratibu kwenye eneo la Igunga tulishindwa kuhamisha matatu na kusababisha njia ya bomba kuhamishwa.

"Tulikaa na jamii wakasema wanayatumia yale makaburi kufanya mila, wale walikuwa viongozi wao, Hanang' pia tumeacha kaburi moja kutokana na masuala ya kiutamaduni," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inaendelea kushirikiana na mradi kuhakikisha makaburi mapya yanayobainika kwenye maeneo ya mradi yanahamishwa kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu fidia, mratibu huyo alisema kuwa hadi Septemba 30 mwaka huu, wananchi 9,858 kati ya 9,927 wametia saini mikataba ya fidia na Sh. bilioni 35.1 sawa na asilimia 99.3 zimelipwa.

"TPDC kwa kushirikiana na EACOP na serikali za mitaa inaendelea kufuatilia wananchi 69 waliobaki ili kukamilisha taratibu za kutia saini mikataba yao ya fidia na hatimaye kulipwa stahiki zao," alisema.

Akizungumzia kuhusu mapato, mratibu huyo alisema serikali inakadiria kupata mapato ya zaidi ya Sh. trilioni mbili kupitia mradi huo.

Alisema mradi huo utapita katika mikoa minane na vijiji 225 na kwa upande wa Tanzania, bomba litakuwa na urefu wa kilomita 1,147, mradi ukitarajiwa kukamilika Julai 2026.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano TPDC, Marie Msellemu, alisema mafunzo ya utekelezaji mradi huo ni muhimu kwa waandishi wa habari ili kurahisisha kufikisha elimu kwa umma kutambua fursa zinazoambatana na mradi.

"Katika ushirikishwaji wazawa kwenye mradi, wamechangamkia mradi na wamekuwa wakishiriki kwenye fursa za mradi ili kujikwamua kiuchumi na kuongeza ukuaji uchumi wa taifa. Wanawake wamejitokeza kwa kiasi kikubwa kuchangamkia fursa," alisema.




Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Cyprian Luhemeja (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kufungua mkutano wa kimataifa wa kujadili matumizi ya zebaki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri atuma timu kuchunguza kashfa katika kampuni ya madini

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya kampuni za wazawa zinazotoa huduma kwa Kampuni ya Shanta Mining, zimeilalamikia kwa kusitisha mikataba nao pasi na kuwapa taarifa.

Kampuni hizo zimedai kuwa zimekuwa zinatoa huduma na vifaa kwa kampuni hiyo ya madini kwa muda mrefu, lakini huu ni mwezi wa tatu hazijapewa kazi (zabuni).

Kutokana na madai hayo, Waziri wa Madini, Antony Mavunde ametuma timu ya watalaamu wa wizara kuchunguza undani wa suala hilo.

Mmoja wa wamiliki wa kampuni hizo (jina tunalihifadhi) aliiambia Nipashe juzi kuwa wamepata taarifa zisizo rasmi kwamba kampuni zao zimewekwa katika orodha ya kutopewa kazi (blacklist) na Kampuni ya Shanta Mining, pasi na kuambiwa kilicho nyuma ya uamuzi huo.

"Sisi tunatambuliwa hadi kwenye Tume ya Madini kwamba tunaipa huduma kampuni hiyo, maana sheria za nchi zinaelekeza kampuni za madini zinapokuwa zinahitaji vifaa au huduma inayozidi Dola 100,000, lazima makubaliano hayo yapitie kwenye Tume ya Madini.

"Tunashangaa kampuni zetu zimeondolewa kwenye orodha ya kupewa kazi za Shanta. Sasa kazi zote anapewa ... (akataja jina la kampuni). Tunajua kampuni hii imesajiliwa Tanzania, lakini wamiliki wake wana asili ya India," alidai.

Aliendelea kudai kuwa hatua iliyochukuliwa ya kuwanyima kazi wazawa, wanahisi italeta madhara si tu kwa kampuni zao, bali hata katika mapato ya madini kutokana na ukiukwaji utaratibu wa 'local content'.

Waziri wa Madini, Mavunde, alipotafutwa na Nipashe jana asubuhi kuzungumzia suala hilo, alisema hakuwa na taarifa za kinachojiri katika katika Kampuni ya Shanta, hivyo akaomba apewe muda afuatilie.

Baada ya saa moja, Waziri Mavunde alitoa mrejesho kwa mwandishi, akisema "nimeeleza timu yangu kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa hizo".

**"Baadhi ya wauzaji kama vile ... na ... (alitaja majina ya kampuni mbili) wameathirika, na majadiliano yanaendelea kutafuta suluhisho.**

Honest Mrema, Mkuu wa Operesheni wa Shanta Mining, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alikiri kampuni yao kusitisha kutoa kazi (zabuni) kwa baadhi ya kampuni za wazawa.

Alisema uamuzi huo imechukuliwa na uongozi wa kampuni ili kupisha uchunguzi wa kihasibu unaoendelea dhidi ya baadhi ya kampuni ambazo wamezihisi kufanya udanganyifu wa kifedha.

Mrema alifafanua: "Hivi karibuni, Shanta imekuwa inaendelea na ukaguzi wa ununuzi na baadhi ya masuala kuhusu ubora, bei na udanganyifu wa kifedha umegundulika.

"Kazi hii bado inaendelea na ripoti kamili itakapotolewa, itawasilishwa pia kwa Tume ya Madini. Kwa sasa, baadhi ya malipo yamezuiwa hadi matokeo ya uchunguzi yatakapojulikana.

"Baadhi ya wauzaji kama vile ... na ... (alitaja majina ya kampuni mbili) wameathirika, na majadiliano yanaendelea kutafuta suluhisho.

"Shanta imejizatiti kutumia wauzaji wa ndani kwani ni faida kubwa, na inahakikisha inazingatia kikamilifu kanuni za 'local content' (kutumia wazawa au kampuni za wazawa katika kupata huduma au vifaa)."

Alipoulizwa na Nipashe kuhusu kampuni inayolalamikiwa kwamba hivi sasa wanaendelea kuipa kazi/ zabuni ilhali wazawa wengine wananyimwa, Mrema alisema "si kampuni zote zinatiliwa shaka. Zipo nyingine zaidi zinaendelea na kazi".

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz




Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Bank of Africa Tanzania, Nandi Mwiyombella (wa pili kulia), akizungumza wakati wa kukabidhi msaada wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 zilizotolewa na benki kusaidia mpango wa "Rafiki wa Amana" unaolenga kuboresha huduma za afya kwenye Hospitali ya Rufani ya Amana, Dar es Salaam jana. Wengine ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Bryceson Kiwelu (wa pili kushoto) na Maofisa Waandamizi wa benki na hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA: Hata tukibaki na mgombea mmoja, hatujitoi Uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Elizabeth Zaya**

UONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) umesema utashiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hata kama kitabakiwa na mtaa mmoja baada ya orodha ya wagombea kuwekwa hadharani.

Umesema hata kama kukitokea changamoto kubwa kiasi gani katika hatua zilizobaki, hakitakuwa tayari kujitoa katika uchaguzi huo.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Arusha na viongozi wa chama hicho, wakiwamo Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara, Benson Kigaila na Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema.

Kigaila alisema kuwa tangu kufunguliwa mlango wa kuchukua na kurejesha fomu, kumekuwa na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo, wanaendelea kufanyia tathmini na watatoa taarifa ya jumla na hatua za kuchukua.

"Lakini ninaomba niwaambie wanachama wetu kwamba pamoja na chagamoto zilizojitokeza, hatutarudi nyuma kama tulivyofanya mwaka 2019. Niwasihi endeleeni kujiandaa, hatutajitoa.

"Tunaendelea kufanya tathmini katika kanda zote nane, tutatoa taarifa kamili kuhusu changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwenye kazi hii ya kuchukua na kurejesha fomu, lakini hata iweje uchaguzi ni lazima tushiriki," alisisitiza Kigaila.

Kwa upande wake Lema alisema sekretarieti ya chama hicho hivi sasa inakusanya taarifa nchi nzima juu ya mwenendo wa uchukuaji na urejeshaji fomu kwa wagombea wake kwa ajili ya kukabidhi kwa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe.

"Baada ya kumaliza kukusanya, tutakabidhi kwa mwenyekiti wetu taifa halafu yeye ndiye atatoa taarifa kamili kwa umma.

"Lakini hata hivyo, kwa wanachama wetu na viongozi wetu kila mahali, wasikate tamaa kuendelea kupigania dhamira yetu. Hata kama tutabaki na wenyeviti watano, na wengine wote kuenguliwa, tutafanya kampeni kama vile tumebaki nao asilimia 90 kama ambavyo tulikuwa tumepanga.

"Chama chetu kabla ya kuanza kuchukua na kurejesha fomu, tulikuwa na wagombea kwa asilimia 87 hadi 92 nchi nzima, wito wangu kwa viongozi wote wa kanda wa chama chetu ni kwamba, hata kama tukibaki na mgombea kwenye mtaa mmoja, twende naye tukafanye kampeni.

"Hatuendi tu kufanya kampeni kwa sababu tunataka kushinda, tunataka kikombe cha dhambi kijae. Na mimi nimefunga na kuomba kwa ajili ya suala hili," Lema alidai.

Kauli hiyo ya CHADEMA imekuja siku moja baada ya Chama cha ACT Wazalendo kusema kinajiandaa kuandika barua kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutaka kurejeshwa katika mchakato wa uchaguzi huo, wagombea wa chama hicho waliokumbana na changamoto wakati wa kuchukua na kurejesha fomu, ikiwamo ofisi husika kunakorejeshwa fomu hizo kutofunguliwa makusudi ili kuwanyima haki yao ya kikatiba.

**Umesema hata kama kukitokea changamoto kubwa kiasi gani katika hatua zilizobaki, hakitakuwa tayari kujitoa katika uchaguzi huo.**

Kwa maoni: +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# Mbunge ahofia ongezeko watoto wanaolala nje kwenye maduka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kilombero (CCM), Abubakar Assenga, amesema kuna ongezeko la watoto wanaolala nje ya maduka usiku kwenye majiji makubwa, wasiowajua wazazi na kutaka kuwapo udhibiti kwa kuweka utaratibu wanaozaa wawajibike kulea.

Akichangia bungeni jana, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya serikali kwa Mwaka 2025/26, Assenga alisema hakuna taifa ambalo litakuwa la kutelekeza watoto barabarani.

"Mheshimiwa Waziri nawaomba sana ni nani anafuatilia ongezeko la watu kwenye nchi yetu? Lakini mheshimiwa mwenyekiti na mawaziri nilienda Mwanza pale na kamati tulikuwa Dar es Salaam tunaangalia TBC inavyorusha watoto wa taifa hili wanavyolala kwenye maduka usiku."

"Watoto wa taifa hili pale Mwanza mimi nimewakuta nawahoji ukiangalia video yangu mtoto hajui baba wala mama sasa kama tunataka kwenda kwenye maendeleo ya kweli na mheshimiwa Msambatavangu alishawahi kusema siku moja hapa lazima tujiulize kijana wa kike na wa kiume wakiamua katika starehe zao kuzaa watawajibika kulea," alisema.

Alitoa mfano juzi akitoka bungeni alikutana na mama mwenye watoto watatu ambaye anadai kila mmoja na baba yake na wamemkimbia.

"Mama yule siku akichoka akatelekeza wale watoto wanahesabika ni maskini wa watanzania, mheshimiwa mwenyekiti haikubaliki tunaomba taasisi zinazohusika msimamie ongezeko letu na mlidhibiti ili kuendana na maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Alimpongeza kijana wa Mbeya aliyeonekana kwenye picha mjongeo akisimamisha vijana wa bodaboda na kuwaambia si ujanja kuzalisha wanawake na kupeleka watoto kwa bibi.

"Kijana anasema analea watoto wake watatu nyumbani kwake na ni bodaboda hata hakimu akinihukumu leo anaweza kunipunguzia adhabu kwasababu nalea mwenyewe, huyu amewakusanya vijana wenzake na kuwaambia we fulani umezalisha watoto wanne umepeleka kwa bibi."

"Unasema wanawake wanaojileta unazalisha tu, watoto wanakwenda mtaani na yatima wamezidi na sasa hivi tuna utamaduni wa kujenga vituo vya watoto yatima na hatulei watoto yatima kwenye nyumba zetu, hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli kama tunaongeza watu kiholela kwa namna hiyo," alisema.

**VIPAUMBELE**

Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Costatine Kanyasu alisema amefanya utafiti mdogo na kugundua kuna tatizo la vipaumbele na miaka ya nyuma vijana walihamasishwa kusoma Sayansi, lakini kwasasa mwanafunzi wa tahsusi ya PCB mwenye ufaulu wa daraja la kwanza yenye alama 1.9 anakosa chuo cha kusomea udaktari.

"Kuna vijana wamekosa vyuo nina mifano ilibidi vijana wengine wabadilishe fani badala ya kusomea udaktari imebidi wakasomee biashara, serikali lazima iangalie hili kwani vyuo vingi vya fani ya afya vinajaa, tunapoteza vijana ambao wamepambana huku chini kwa kisingizio ambavyo havieleweki, kwanini serikali isiongeze vyuo vya madaktari kama imegundua Muhimbili na UDOM vimejaa, kwanini kisianzishwe chuo kikubwa cha udaktari," alihoji.

Alisema suala la kulazimisha kubadili fani walizopanga kusoma matokeo yake wanaandaa kundi ambalo siku za usoni linakuja kuwa ni tatizo.

**KILIMO**

Mbunge wa Bukene (CCM), Selemani Zedi, alishauri mpango kuendelea kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuwa ni eneo linalochukua Watanzania wengi.

"Ukitaka kuinua maisha ya wananchi wetu hakuna jingine zaidi ya kuongeza tija kwenye kilimo ambapo huwezi kukwepa kutumia mbegu za kisasa na mbolea, bado kuna mahitaji makubwa ya matumizi ya mbolea hivyo naunga mkono mapendekezo ya mpango kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu ili kuongeza tija kwenye kilimo lazima tulime kwa kutumia mvua na kutumia skimu za umwagiliaji," alisema.

Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi alisisitiza serikali iendelee kuwekeza kwenye kilimo ili kufikia malengo ya mpango kwa urahisi ikiwa ni pamoja na uchumi jumuishi, kuongeza pato la taifa na ajira.

"Tuwekeze zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji, tuangalie maeneo ambayo tayari yana rasilimali maji tayari, ni namna gani tumeshayatumia maeneo haya, tufanye kilimo cha umwagiliaji chenye tija, wananchi watoke kwenye kilimo cha mkono na kuingia kwenye kilimo cha kisasa ili kukabiliana na tatizo la ajira, tuna hekta zaidi ya 4,000 ambazo zinaweza kufanyiwa kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Kadhalika, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda, alisema suala la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni muhimu na kuomba fedha iongezwe kwenye hilo ili kupata wataalamu wengi bila kusahau ujuzi kwenye akili mnemba.

## HABARI KITAIFA

# TANROADS yatoa ufafanuzi bil. 18/- za matengenezo miundombinu BRT

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam unatekeleza mradi wa matengenezo ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) awamu ya kwanza chini ya mradi wa OPBRC uliotiwa saini rasmi tarehe 7 Septemba 2018.

Mradi huu ni wa muda mrefu; ulianza rasmi tarehe Mosi Aprili 2019 ukitekelezwa na mkandarasi M/s Bharya Engineering & Contracting Co. Ltd (BECCO) kwa muda wa miezi 60, yaani miaka mitano.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam, John Mkumbo, alitoa ufafanuzi huo jana na kueleza kuwa mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 18.509 ambazo zinajumuisha makundi matatu ya kazi na si mradi wa Jangwani pekee.

Aliyataja makundi hayo kuwa ni pamoja na mradi wa matengenezo ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya kwanza yenye urefu wa kilomita 21.4 ukihusisha barabara ya Morogoro kuanzia Ferry mpaka Kimara Mwisho, barabara ya Kawawa (Magomeni Mapipa - Morocco) na barabara ya Msimbazi (Fire - Msimbazi BRT Station).

Mkumbo alisema kuwa TANROADS pia inatekeleza kazi za maboresho ya sehemu zilizoharibika, ikihusisha matengenezo makubwa ya tabaka la lami katika sehemu zilizokuwa zimeharibika.

Maeneo yaliyofanyiwa marekebisho ni Ubungo Maji, Kibo, Corner, Baruti, Bucha, Korogwe na Kimara Mwisho. Tabaka la lami katika maeneo haya liliondolewa (milling) pamoja na kuwekwa lami mpya kwa kutumia teknolojia ya Superpave (SP 12.5), kuweka nguzo za zege (precast concrete poles C20/guard posts), ujenzi wa sehemu za watembea kwa miguu (paving blocks), ujenzi wa kingo za barabara (kerbstones) na matengenezo kwenye njia za waendesha baiskeli.

Alisema TANROADS Dar es Salaam pia imefanya kazi za dharura. Kazi hizi zinahusisha matengenezo ya uharibifu ambao haukutarajiwa. Kazi hizi ni pamoja na kuondoa tope, mchanga na takataka kwenye daraja na eneo la barabara wakati wa mafuriko na mvua kubwa na matengenezo ya miundombinu yatokanayo na ajali za barabarani kwenye miundombinu ya BRT awamu ya kwanza.

Mkumbo alieleza kuwa kazi za matengenezo zimefanyika wakati wote. Kazi hizo zinahusisha; urudishiaji wa michoro ya barabara (road marking), uwekaji wa alama za barabarani, matengenezo/uzibuaji mitaro ya maji ya mvua ndani ya uwanda wa Km 21.4 za mradi, kuweka mifuniko ya zege kwenye mifumo ya maji, kuondoa mchanga kwa kufagia barabara ndani ya Km 21.4 kila siku.

Kazi zingine, meneja huyo alisema ni pamoja na kufyeka majani na kutunza maeneo yenye bustani ndani ya eneo la mradi, kuondoa vichaka na kupunguza miti iliyo pembezoni mwa barabara, kuziba viraka/mashimo, matengenezo madogo ya madaraja yaliyomo ndani ya mradi, marekebisho ya njia za waenda kwa miguu/baiskeli, matengenezo ya nguzo za zege zinazoharibika, matengenezo ya maungio ya zege, marekebisho ya mifuniko na kuzibua mifereji yote iliyo katika eneo la mradi.

# Dodoma yaipiku Dar kwa matumizi dawa za kulevya

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imeutaja mkoa wa Dodoma sasa unaongoza kwa matumizi ya dawa za kulevya, ikiwamo Heroine, ukifuatwa na Dar es Salaam.

Mei 17 mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya dawa za kulevya kwa mwaka 2023, alisema Dar es Salaam ilikuwa inaongoza kwa matumizi na asilimia 78 ya watumiaji walikuwa vijana.

Kamishna wa DCEA, Peter Patric, aliiambia Nipashe siku chache zilizopita kwamba mikoa inayofuatia kwa kuwa na idadi kubwa ya matumizi ya dawa hizo ni Mwanza, Arusha na Mbeya.

Pia alisema dawa za kulevya zinazoongoza kwa kutumika zaidi nchini ni bangi, mirungi, heroin, cocaine na tiba zenye asili ya kulevya ambazo zinatumika pia hospitalini, licha ya kwamba baadhi huzitumia kama kilevi.

"Aina nyingine ni 'methamphetamine' ambazo tumeanza kuzikamata hivi karibuni na zilianza kuingia nchini kwa wingi mwaka 2021 na mwaka jana tulikamata zaidi ya tani mbili," alisema Patrick.

Alisema asilimia 85 ya heroine inayotumika duniani inatoka Afghanistan na wanatarajia mwaka huu na ujao kiwango hicho kitashuka kwa sababu Kundi la Talbani baada ya kuchukua madaraka na kuongoza eneo hilo wamepiga marufuku kilimo cha 'Pop Plant' ambalo ndio zao linalozalisha dawa hiyo.

Aidha utafiti unaonesha kwamba karibu asilimia 36 ya watu wanaotumia dawa hizo kwa njia ya kujidunga wanaishi na Virusi vya Ukimwi (VVU).

Alisema wanawake wanaonekana kuathirika zaidi kwasababu utafiti unaonesha kati ya 100 wanaojidunga angalau 60 walikuwa wanaishi na VVU, na kwamba asilimia 90 ya tabaka hilo wanaotumia dawa za kulevya wanafanya biashara ya ngono ili waweze kupata fedha ya kununulia dawa.

Alisema wameweka mikakati mbalimbali ikiwamo kupunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini,

Vile vile, wameweka mikakati ya kupunguza na kumaliza kabisa mahitaji ya dawa za kulevya kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yake ili umma usijiingize kwenye matumizi ya dawa hizo.

"Mikakati hiyo pia ni kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini," alisema Patrick.




## CONTRACTORS REGISTRATION BOARD

## SUSPENSION OF CONTRACTORS

The Contractors Registration Board (CRB) is a statutory regulatory Board established in accordance with the Contractors Registration Act Cap 235 (R.E) 2002 to register all types of contractors, and regulate their conduct for protecting consumers of construction services in Tanzania. In executing this objective, CRB is also duty bound to promote development of local contractors across the country.

CRB wishes to inform all Clients (developers), Consultants and the General Public that the following contractors have been suspended from practising as Contractors with effect from 01.11.2024 in accordance with Sections 13 and 15 of the Contractors Registration Act Cap. 235 (R.E) 2002. The key reason for suspension is failure to make good indebtedness arising from the Contractors Assistance Fund (CAF).

| S/N | COMPANY NAME | CATEGORY | REG NO: |
|---|---|---|---|
| 1. | SAMCAT (T) LIMITED | BUILDING | B1/0109/09/2010 |
| | | CIVIL | C3/0076/09/2010 |
| 2. | SAMNA (T) INVESTMENTS LIMITED | BUILDING | B2/140/07/2022 |
| | | CIVIL | C4/496/07/2022 |
| 3. | VISION SCOPE LIMITED | BUILDING | B5/1204/08/2018 |
| | | CIVIL | C4/1018/09/2018 |
| 4. | CAPITAL NETWORK LIMITED | BUILDING | B5/0439/10/2009 |
| | | CIVIL | C5/0391/10/2009 |
| 5. | MAJOR CONSULTANTS LIMITED | BUILDING | B7/4191/02/2014 |
| | | ELECRICAL | E6/0111/04/2014 |
| | | SPECIALIST | SPE3/0627/01/2014 |
| | | CIVIL | C6/1360/12/2013 |

**REGISTRAR**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ni muhimu kufahamu visababishi vya kupoteza kumbukumbu

**WATAALAMU** bingwa na bobezi wa magonjwa, afya ya akili na mfumo wa fahamu, kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, wametoa ufafanuzi namna ubongo wa binadamu unavyofanya kazi na kuhifadhi kumbukumbu.

Ingawa wana angalizo kwamba wanaopoteza kumbukumbu, wanaweza kusababishiwa na magonjwa ya akili kama vile msongo wa mawazo, lakini vilevile kupotea kwa kumbukumbu mbaya, ni tiba ya asili ya kiungo hicho muhimu kwa mwili wa binadamu.

Wataalam wanaeleza mfano mtu anaposhuhudia mauaji ya kikatili huwa haitoki kwenye kumbukumbu yake na tiba itakayomfaa ni kupoteza kumbukumbu.

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu kutoka hospitali hiyo, Dk. Damas Mlaki, anasema jamii inapaswa kuzingatia elimu kuhusu afya ya akili kwa manufaa ya ustawi wa jamii kwa ujumla.

Magonjwa yanayohusisha ubongo kutofanya kazi yake ipasavyo ni msongo wa mawazo pia kiharusi na waliojeruhiwa sehemu fulani ya ubongo kutokana na ajali na kukwamisha utendaji kazi wa ubongo ipasavyo.

Kadhalika, wapo ambao hupata athari hasa kupoteza kumbukumbu za masuala mbalimbali ambazo ubongo kwa mfumo wake thabiti, huzihifadhi kwa matumizi ya baadaye.

Msongo wa mawazo, sononа, watu kupitia na kuishi kwenye changamoto za maisha ambazo hazipati ufumbuzi wa mapema, huuathiri ubongo na kuhitaji kupewa matibabu ya dawa ama ushauri.

Mbinu za kujikinga na namna ya kufanya ubongo utunze kumbukumbu, inaelezwa kuwa ni kufanya mazoezi ya kimwili na kiakili, lishe bora na kupata usingizi wa kutosha usiopungua saa nane.

Inashauriwa watu kuzingatia usingizi ili kurejesha kumbukumbu na wanafunzi wanapewa angalizo la kutoa muda wa kujisomea kwa kuupumzisha ubongo kwa kupata usingizi jambo ambalo ni muhimu.

"Wanaokesha, wanafunzi kusoma bila kuupa nafasi usingizi ni tatizo. Wanaweza hata wanachokisoma wasikikumbuke katika chumba cha mtihani. Inahitaji ulale angalau saa nane kwa siku, ili kuzihuisha kumbukumbu."

Mbinu nyingine ya kutunza kumbukumbu ni kuupa ubongo mazoezi ya kiakili, wataalamu wanasisitiza pia kuangalia filamu, kusoma vitabu, gazeti, kucheza michezo ya asili kama bao, kwa sababu mtu anatumia fikra ili kumshinda mwenziwe.

Wito wa watalaam hao ni jamii izingatie ushauri wa wataalamu wa afya, ili kuboresha ustawi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.


Vilevile, jamii iache unyanyapaa kwa ambao uwezo wao wa ubongo na kutunza kumbukumbu ni duni hasa watoto, ambao wanapokuwa masomoni hushindwa kufikia wastani wa juu, kwa matamanio ya wazazi au walezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, aliwahi kusema jamii hasa familia, iache kufananisha uwezo wa ubongo baina ya mtoto mmoja na nduguze, kwani ni kawaida kutofautiana kutokana na ubongo ulivyoendelezwa.

Utafiti unaofanywa maeneo tofauti duniani unaonesha kuwa, uwezo wa ubongo kati ya binadamu mmoja na mwingine hutofautiana, licha ya kuwa pengine wana rika sawa hata kama watoto wa familia moja.

Jamii inatakiwa kuacha kumsema vibaya mtoto mwenye uwezo mdogo hata kumnyanyapaa na ni vyema ubongo wa watoto hao ukaanza kuendelezwa mapema ili kukuza nafasi ya kutunza kumbukumbu za wanachojifunza hata kukuza vipaji vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Restuta James

## Serikali inanyanyasa raia wake kwa kutolipa madeni

**IJUMAA** iliyopita, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Oran Njeza, analiambia bunge kwamba hadi Juni 2023, madeni ya makandarasi yaliyokuwa yamehakikiwa yalikuwa na thamani ya Sh. trilioni 3.03.

Anasema pia kuwa ambayo hayajahakikiwa yalikuwa Sh. bilioni 64.72. Njeza anafafanua athari za malimbikizo ya madeni hayo zimeonekana kwenye sekta ya barabara, maji, kilimo na mifugo, ambazo zimeshindwa kutekeleza miradi mipya.

Wiki hii Jumatatu, wabunge pia wanaibana serikali na kuitaka iwalipe wazabuni, ambao wengine wana madai ya muda mrefu na wanaelekea kufilisika.

Hii ni habari mbaya kwa wazabuni hasa wenye madeni ya muda mrefu. Kila mara tumesikia viongozi wa ngazi mbalimbali serikalini, wakijinasibu kuanzisha miradi kadha wa kadha, wakieleza kupeleka huduma kwa wananchi, wakitamba makusanyo ya mapato kuongezeka, lakini inawafilisi wafanyabiashara waliokubali kufanya nayo kazi.

Tumeshuhudia katika baadhi ya maeneo, ujenzi wa barabara ukiwa umesimama kwa sababu mkandarasi ameshindwa kuendelea na mradi, baada ya kuishiwa na serikali kutomlipa kwa wakati.

Tafsiri yake ni kwamba, mradi ambao mathalani ungetekelezwa kwa mwaka mmoja, utatekelezwa kwa miaka miwili au zaidi.

Siyo hivyo tu, miradi ambayo ingetakiwa kuanzishwa mwaka huu, nayo itasubiri hadi mwakani au miaka mingine kadhaa.

Wakati miradi ikikwama au kuchelewa kuanza, wafanyabiashara nao wanafilisika kwa kucheleweshewa malipo. Ucheleweshaji unaua kampuni kubwa hadi viwanda vidogo na biashara ndogo mtaani.

Kwa mfano, kuna wale wazabuni wadogo ambao yamkini wazabuni wanaolisha shule, wanachukua unga, maharage, mchele, mafuta au chumvi, kwao. Hawa nao wanaumia mno.

Hebu tujiulize, kungekuwa na mzunguko wa fedha kwa kiasi gani kama Sh. trilioni 3.03 zingeingia kwenye mifuko ya wazabuni.

Benki zingekuwa na mzunguko mkubwa kiasi gani kama fedha hizi zingelipwa? Hatuwezi kujinasibu kukuza uchumi na kuwezesha wananchi kiuchumi, wakati hatuwalipi wazabuni.

Kama fedha hizi zingelipwa, maana yake ni kwamba watu wangepanua wigo wa uwekezaji, wafanyakazi walio kwenye mzunguko wa ukandarasi wangejenga nyumba au wangefungua biashara na hivyo fedha hiyo ingefika kwa wananchi wengi zaidi.

Matokeo ya serikali kuchelewesha malipo hayo, yanakausha sio tu kipato kwa makandarasi ambao wanaweza kuwa ni watu wenye kipato cha kati hadi cha juu, bali cha hohehahe ambao wangeuza vitumbua, mihogo na chai ya rangi kwenye miradi hii, wauza matofali, mchanga na kokoto, ambao wangeongeza kipato kwa wajenzi wapya wa nyumba na ukuaji wa kampuni za wazabuni hao.

Ni Septemba mwaka huu, ambayo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilitangaza kuvuka lengo la makusanyo hadi Sh. trilioni 2.34 kwa mwezi Julai ikiwa ni zaidi ya lengo lililowekwa kwa asilimia 104.4, kukusanya Sh. trilioni 2.246.

Taarifa njema za makusanyo ya mapato zinapotolewa, ziwekewe mazingira ya kulipa wazabuni na kipekee wa ndani, ili kurejesha fedha kwenye mzunguko.

Kutolipa kwa wakati siyo tu hatuwatendei haki wazabuni bali hatuitendei haki nchi yetu, ambayo ina nafasi ya kupiga hatua ya maendeleo, kwa mwananchi mmoja mmoja na nchi kwa ujumla; ni suala la kujipanga vizuri.

Wako wazabuni waliokopa benki, wanatakiwa marejesho na riba inaongezeka, kitendo cha kutolipwa, wananyanyaswa na kibaya zaidi, anayefanya hivyo ni serikali yake.

## 22,840 waliokatisha masomo warejea shuleni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Machi 2024, wanafunzi 22,844 waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, wamejiunga tena kuendelea na masomo.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa anajibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Fatma Toufiq.

Mbunge huyo alitaka kujua idadi ya wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kujifungua tangu serikali itoe rukhsa wanafunzi hao kuendelea na masomo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema serikali ilitoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

"Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya wanafunzi waliojiunga tena na shule baada ya kukatiza masomo walikuwa 22,844 ambapo kupitia mfumo rasmi ni 5,142 na mfumo usio rasmi ni 17,702," alisema.

Naibu Waziri Kipanga alisema kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa wanafunzi wa kike, serikali kupitia wizara hiyo inaendelea kusimamia utekelezaji waraka tajwa ili kuhakikisha wanafunzi waliopata ujauzito, wanarejea shuleni na kutimiza ndoto zao kielimu.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema idadi hiyo ni kubwa na kuhoji mkakati wa serikali kuhakikisha idadi hiyo inapungua - wanafunzi wasipate ujauzito.

"Wanafunzi wanaonyonyesha, utaratibu wao upoje wanapokuwa wanaendelea na masomo?" mbunge huyo alihoji.

Kipanga, akijibu maswali hayo, alisema serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kupunguza au kuondoa tatizo la wanafunzi kupata ujauzito.

"Kwenye maeneo ambayo tumeona yana changamoto kubwa tunahakikisha kunakuwa na mabweni kwa ajili ya vijana wetu, hasa watoto wa kike kuondoa suala la kwenda (shuleni) na kurudi (nyumbani).

"Kila taasisi ya elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu tunakuwa na madawati maalumu ambayo yanatoa ushauri na unasihi kuhusu makuzi na mabadiliko ya kimwili," alisema.

Aliongeza kuwa mkakati mwingine ni kuanzisha somo la maadili na linaanza kufundishwa kupitia mtaala mpya wa elimu na serikali itaendelea kusimamia sheria na taratibu ili kuchukua hatua kali kwa wanaofanya vitendo vya unyanyasaji na kuwapatia ujauzito wanafunzi.

"Kwa wale wanaorudi shuleni katika kuhakikisha hatuathiri makuzi ya watoto wa wanaosoma, waraka umetoa mwongozo namna ya kumlea mtoto kwenye mazingira mazuri na kwenye shule vimeanzishwa vyumba ambavyo watoto hao wanalelewa huku wazazi wao wakiendelea na masomo," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Chakechake (CCM), Maryam Azan Mwinyi alihoji mkakati wa serikali wa kuwapa posho wanafunzi hao ili wabaki shuleni.

Kipanga akijibu swali hilo, alisema serikali imebeba ushauri huo na watafanyia tathmini kuangalia kama suala hilo linatekelezeka au la.



Mtambo ukishusha vyuma kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la daraja la Mlalakuwa, Mwenge, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TAKUKURU yabaini upigaji mamilioni katika miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Singida imebaini upigaji mamilioni ya shilingi kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Manispaa ya Singida ambako wazabuni wamekuwa wanapatiwa 'malipo hewa'.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Sipha Mwanjala, akizungumza jana na waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2024, alisema kutokana na malipo hayo hewa, zimeokolewa Sh. milioni 20.3.

Alisema kuwa katika mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto na jengo la dharura katika Hospitali ya Manispaa ya Singida, malipo hewa yalifanyika kwa mzabuni aliyepeleka matofali 43,500 lakini akalipwa fedha za matofali 48,000 na hivyo Sh. 1,732,500 zilizidishwa.

Mwanjala alisema kuwa katika ujenzi wa Kituo cha Afya Mtipa, Manispaa ya Singida, zimeokolewa Sh. milioni 10.9 baada ya kubainika baadhi ya ununuzi wa vifaa ulifanyika kwa bei ya juu kuliko bei iliyopo sokoni.

"Sh. 225,000 zilirejeshwa baada ya kubainika kuwa malipo yalifanyika kwa mzabuni kwa ajili ya kuleta vifaa vya vioo vya choo lakini hakuvileta. Pia Sh. milioni 4.9 ziliokolewa kwenye mradi wa upanuzi wa mzani wa Mughamo, Manispaa ya Singida," alisema.

Mwanjala alisema kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Sh. milioni 3.2 zilikatwa katika mradi wa ujenzi wa bweni la watoto wenye mahitaji maalumu Shule ya Msingi Darajani kama kodi ya zuio, lakini hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema kuwa katika mradi huo, vifaa vyenye thamani ya Sh. 1,726,900 pia vililipiwa lakini havikupelekwa eneo la mradi.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Sh. 1,450,000 ziliokolewa kupitia ufuatiliaji wa miradi miwili ya ujenzi wa Zahanati ya Mukulu, jengo la mama na mtoto na jengo la kuhifadhi maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Kiomboi.

"Katika Hospitali ya Wilaya ya Kiomboi, mzabuni alipewa fedha ya kutengeneza madirisha ya aluminium 45 wakati yaliyohitajika ni 44, hivyo Sh. 250,000 zilizidishwa na katika mradi wa zahanati ya Mukulu, milango minne haikuwa na vipimo sahihi vyenye thamani ya Sh. milioni 1.2, ilibadilishwa," alisema.

Mwanjala alisema kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ua Ikungi, Sh.154,200 ziliokolewa katika mradi wa ujenzi wa darasa na matundu ya vyoo vya wasichana katika Shule ya Sekondari Minyughe ambazo zilikuwa ni fedha za kodi ya zuio bila kupelekwa TRA.

Alisema kuwa katika kipindi hicho cha Julai hadi Septemba 2024, TAKUKURU ilipokea malalamiko 78. Kati yake, 53 yalihusu vitendo vya rushwa na 25 hayahusu vitendo vya rushwa.

"TAKUKURU Mkoa wa Singida inatoa rai kwa wananchi wote kujiepusha na vitendo vya rushwa na kushiriki kikamilifu katika kuzuia katika kipindi hiki cha mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA NISHATI
## MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

### MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mpanda Filling Station, S.L.P 113, Shinyanga. | Kiwanja Na. 229, Eneo la Kasimba, Mpanda, Katavi. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 2. | katisunga fuel filling station, S.L.P 688, Mpanda. | Kijiji cha Katisunga, Mpanda, Katavi. | Said Salula Gacha (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 3. | Sumosa Filling Station and Company Limited, S.L.P 84, | Kiwanja Na. 811, Kitalu "B", Eneo la Isungilunde, | Suleiman Suleiman (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| | Sikonge. | Sikonge, Tabora. | | |
| 4. | New Mchenya Petroleum Co. Ltd, S.L.P 113, Shinyanga | Kiwanja Na. 23, Kitalu "B", Eneo la Songambele, Shinyanga. | Cosmas Juma Mchenya (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 165, Kitalu "L", Moshi, Kilimanjaro. | Hilmi Ahmed Mbaraka (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 6. | Ndomba Filling Station, S.L.P 355 , Handeni. | Kijiji cha Kang`ata, Handeni, Tanga. | John Stephen Ndomba (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | Optimal Energy (T) Ltd, S.L.P 80042, Dar es Salaam. | Eneo la Sagamaganga, Kilombero, Morogoro. | Guled Aden Kassim (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Amasha Venance Mgaya, S.L.P 22, Ulanga. | Eneo la Minepa, Ulanga, Morogoro. | Amasha Venance Mgaya (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | Evosha Trading Company Limited, S.L.P 13134, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P3636, Eneo la Mbezi Makabe, Ubungo, Dar es Salaam. | Gaspar Casmiry Ngalu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 10. | Alphonce August Ngowi, S.L.P 67315, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P19728, Kimara, Ubungo, Dar es Salaam. | Alphonce Augustino Ngowi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 11. | Nyaishozi Oil Limited, S.L.P 178, Karagwe. | Kiwanja Na. 10, Kitalu "A", Eneo la Kwa Mathias, Kibaha, Pwani. | Wilson Boniphace Bagoka (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Makarios Limited, S.L.P 68238, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 468, Kitalu "A", Kongowe, Kibaha, Pwani. | Elinyisia Titus Kipokola (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 13. | Puma Energy Tanzania Limited – Puma Mtwara Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 813, Kitalu "B", Mikindani – Magomeni, Mtwara. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 14. | Nocha Sebe Samwel, S.L.P 68006, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 618, Kitalu "C", Eneo la Mshikamano, Musoma, Mara. | Nocha Sebe Samwel (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 15. | Tropical Helicopters Limited, S.L.P 627, Arusha. | Kijiji cha Migandini, Arumeru, Arusha. | Benjamini John Simpson (Raia wa Kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 16. | Tanzania Breweries Limited – Arusha Plant, S.L.P 3103, Arusha, | Kiwanja Na. 14238, Eneo la Viwanda, Arusha. | Michelle Nicola Kilpin (Raia wa Afrika Kusini) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 17. | Lake Oil Limited – Njiro Petrol Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 355, Kitalu "G", Eneo la Njiro, Arusha. | Khazed Hassan Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Total Tanzania Limited – Jacaranda Service Station, S.L.P 1503, Dar es Salaam. | Barabara ya Mahakamani, Eneo la Philips, Arusha. | Mamadou Ngom (Raia wa Senegali) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Kado & Sons Company Limited – Kado Filling Station, S.L.P 52, Monduli. | Kiwanja Na. 334, Eneo la Sinoi, Monduli, Arusha. | Abdusatar Hamis Shaban (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Israel Samwel Ginduri, S.L.P 63, Loiliondo - Arusha. | Kijiji cha Lopolun, Ngorongoro, Arusha, | Israel Samwel Ginduri (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Kuringe Transport Company Limited, S.L.P 50, | Kijiji cha Mundarara, Longido, Arusha. | Liberatus Silvester Temu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| | Sanya Juu. | | | |
| 22. | Nambis Petrol Station, S.L.P 342, Karatu. | Kiwanja Na. 1247, Kitalu "G", Karatu, Arusha. | Yuda Jacob Ombay (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Itracom Feltilizers Limited - Babati, S.L.P 1299, Babati - Manyara. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "A", Eneo la Vilima Vitatu, Babati, Manyara. | Nazaire Nduwimana (Raia wa Burundi) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 24. | Mount Meru Petroleum Limited – Maisaka "B" Petrol Station, S. L. P 7094, Arusha. | Kiwanja Na.1406, Kitalu "R", Maisaka "B", Babati, Manyara. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Valentino Edwardi Nywage T/A Nywage Oil – Kijungu Petrol Station, S.L.P 49, Kongwa – Dodoma. | Kijiji cha Kijungu, Kiteto, Manyara. | Valentino Edwardi Nywage (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Mount Meru Petroleum Limited – Same Petrol Station, S. L. P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 54, Kitalu "K", Same, Kilimanjaro. | Atul Mital (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Elagas Company Limited, S.L.P 41, Moshi. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "X", Eneo la Kiusa, Moshi, Kilimanjaro | Emmanuel Mero (Raia wa Tanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 28. | Mohamed Hussein Mohamed – Kikunde Petrol Station, S.L.P 103, Kibaya – Kiteto. | Kijiji cha Kikunde, Kilindi, Tanga. | Mohamed Hussein Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Adam Filling Station and Company Limited – Ipole, | Kijiji cha Udongo, Sikonge, Tabora. | Yusuph Seleman Nasssor (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| | S.L.P 84, Sikonge. | | | |
| 30. | Dear Mama Filling Station, S.L.P 1234, Kigoma. | Kiwanja Na. 790, Kitalu "A", Eneo la Kihinga, Kigoma. | Jairos N. Hiliza (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 4, Kitalu "U", Eneo la Nyasubi, Kahama, Shinyanga. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Lake Oil Limited - Mkamba, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Ifakara, Kilombero, Morogoro. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Costantine Joseph Mkenda, S.L.P 67129, Morogoro. | Kiwanja Na. 71, Eneo la uwanja wa Taifa, Morogoro. | Costantine Joseph Mkenda (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 34. | Ibra Filling Station, S.L.P 3073, Dodoma. | Kiwanja Na. 58, Kitalu "R", Eneo la Ipagala, Dodoma. | Ibrahim Hassan Mfalla (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Iyegu Limited, S.L.P 37, Kongwa. | Kijiji cha Mlali, Kongwa, Dodoma. | David Yonah Mngurumi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Sadah Moshi Ngereza T/A Mitundu Filling Station, S.L.P 8405, Moshi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "C", Eneo la Mitundu, Manyoni, Singida. | Sadah Moshi Ngereza (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Wilson Ruben Mpinga Mkalama, S.L.P 1007, Mkalama. | Eneo la Nkungi, Mkalama, Singida. | Wilson Ruben Mpinga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Juma George Magere T/A Magere Oil, S.L.P 2402, Iringa. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "D", Eneo la Igingilanyi, Iringa. | Juma George Magere (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | Tanzania Steel Pipes, S.L.P 5476, Dar es Salaam. | Eneo la viwanda la Ubungo, Ubungo, Dar es Salaam. | Yun Chin (Raia wa China) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 40. | Haleluya Wilfred Kessy T/A GP Nanenane Petrol Station, S.L.P 3073, Dodoma. | Kiwanja Na. P17461, Eneo la Mikwambe Toangoma, Temeke, Dar es Salaam. | Haleluya Wilfred Kessy (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Masry Energy Co. Limited, S.L.P 22009, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 16, Kitalu "D", Kivule, Ilala, Dar es Salaam. | Abdallah Silaji Athumani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 42. | Ghcom Company Limited, S.L.P 79941, Dar es Salaam. | Eneo la Saranga, Ubungo, Dar es Salaam. | Genes Apolinary Ng'oja (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 43. | Alex Sabas Silayo T/A Zebra Gas, S.L.P 53040, Dar es Salaam. | Eneo la Kibo, Ubungo, Dar es Salaam. | Alex Sabas Silayo (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 44. | BFS Company Limited, S.L.P 90567, Pwani. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "E", Eneo la Kiluvya, Kisarawe, Pwani. | Godfrey. G.Shirima (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 45. | FAB Energy Company Limited-Pera, S.L.P 70419, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "D", Eneo la Pera, Chalinze, Pwani. | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 46. | Ngerengere Airbase Investment Limited, S.L.P 50, Bagamoyo. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "B", Eneo la Ubena Zomozi, Bagamoyo, Pwani. | Steward Danford Ziguye (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 47. | Bright Vision Limited, S.L.P 72539, Pwani. | Eneo la Vikindu, Mkuranga, Pwani. | Dickson Luwumba (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 48. | China Civil Engineering Construction Corporation, S.L.P 4083, Busega. | Eneo la Kabita, Busega, Simiyu | Dong Haipeng (Raia wa China) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 49. | Maboto Oil, S.L.P 10316, Mwanza. | Kiwanja Na. 137, Kitalu "A", Eneo la Kanyama - Kisesa, Magu, Mwanza. | Robert Chacha Maboto (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Juma Katwale Ndilima T/A Ndilima Oil, S.L.P 88, Ngudu. | Kiwanja Na. 347, Kitalu "B", Eneo la Hungumalwa, Kwimba, Mwanza. | Juma Katwale Ndilima (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51. | Majimoto Filling Station, S. L. P 176, Serengeti. | Eneo la Majimoto, Serengeti, Mara. | Amosi Nyamaroli Giringai (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 52. | Mbwilo FM Company Limited – Chalangwa, S.L.P 124, Chunya. | Kijiji cha Chalangwa, Chunya, Mbeya. | Frank Issa Mbwilo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 53. | Mazwi Trading Company Limited – Makutano Petrol Station, S.L.P 170, Sumbawanga. | Kiwanja Na. 121, kitalu "UU", Eneo la Makutano, Sumbawanga, Rukwa. | Mohammed R. Sumry (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizihilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

# Batilda ataka utulivu uchaguzi serikali mitaa, vijiji, vitongoji

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, amewataka wakuu wa wilaya na wasimamizi wa uchaguzi mkoani hapa kuhakikisha upigaji kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba 27, mwaka huu, unafanyika kwa utulivu wa asilimia 100.

Dk. Batilda alitoa maelekezo hayo jana, baada ya kukagua maandalizi ya uchaguzi huo katika halmashauri za wilaya na mji wa Handeni, akiwa ameambatana na ujumbe wake, akiwamo Katibu Tawala Mkoa, Pili Mnyema, Kamati ya Usalama na Kamati ya Uratibu wa Uchaguzi ya mkoa.

Alisema mafanikio yaliyofikiwa kuandikisha asilimia 110.82 ya wapiga kura na kushika nafasi ya pili kitaifa, yamepongezwa na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, hivyo kuibua haja ya kuhakikisha watu wote wanapiga kura.

Alisema tofauti na uandikishaji uliofanyika kwa siku 10, upigaji kura utatumia saa 10 katika siku moja, hivyo mikakati ya hamasa, ushawishi na kuwapo mazingira bora yanayowavutia watu wengi kwenda kupiga kura inapaswa kutumika.

"Tumefanikiwa kuandikisha wapiga kura kwa asilimia 110.82 kwa zoezi lililofanyika kwa siku 10, sasa tuna saa 10 tu kwa siku moja kuhakikisha kila aliyejiandikisha anapiga kura ili tuuheshimishe uchaguzi huo na kumheshimisha Rais Samia," alisema Batilda.

Aliwakumbusha wasimamizi wa uchaguzi kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili ufanyike na kuthibitika pasipo shaka kuwa ni wa wazi, huru na haki.

Alisema ni dhamira na utashi wa kisiasa wa Rais Samia kuona uchaguzi huo unatoa fursa pana kwa kila raia, kutumia haki yake ya kikatiba kugombea na kumchagua kiongozi anayemtaka.

Dk. Batilda, alisema pamoja na kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo, wasimamizi hao na wakuu wa wilaya wanapaswa kushughulikia na kuondoa changamoto ili upigaji kura ufanyike kwa wepesi na haraka.

Alitoa mfano kuwa mahali penye idadi kubwa ya wapigakura, viongozi hao wanaweza kufuata taratibu kwa kuongeza idadi ya vituo kabla ya Novemba 7, mwaka huu kwa kuwashirikisha wadau hususani vyama vya siasa.

Alisema mazingira ya siku ya uchaguzi yanaweza kuathiriwa na hali ya hewa, kama vile kuwepo mvua ama jua kali, hivyo upo umuhimu wa kuandaa maturubai kukabiliana nayo.

"Tukiyafanya haya na kwa kuzingatia 4R (maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya), tukafanikisha uchaguzi huu, tutakuwa tumemheshimisha Rais Samia na kuuheshimisha uchaguzi huu," alisisitiza mkuu huyo wa mkoa.

Awali, Mnyema, alisema pamoja na mafanikio yanayoonekana kwenye taarifa za halmashauri hizo, Mkuu wa Mkoa na timu zake, afanya ziara hizo ili kujiridhisha na uhalisia uliopo kisha kusaidia utatuzi wa changamoto zinazojitokeza.

# Majaliwa ataka nchi imara Afrika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewataka mameneja na wasimamizi wa rasilimali watu kuwapatia mafunzo watumishi wao mara kwa mara ili nchi za Afrika ziwe imara na maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa jijini hapa na kusema rasilimali watu inayosimamiwa vizuri ni tunu na uti wa mgongo wa maendeleo kwa kila nchi duniani.

Majaliwa aliyasema hayo wakati akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kufungua mkutano wa tisa wa Mtandao wa Mameneja na Wasimamizi wa Rasilimali Watu katika Sekta ya Umma Afrika (APS-HRMnet) wenye kauli mbiu 'Uhimilivu wa Utawala na Ubunifu Kukuza Sekta ya Umma yenye Uelekeo wa Baadaye Kupitia Uongozi wa Rasilimali watu.'

"Rasilimali watu katika utumishi wa umma umekuwa ni nyenzo muhimu ambapo serikali ya nchi husika inaitumia kufia wananchi wake katika kutoa huduma za kiuchumi, kijamii kukuza ustawi wa jamii husika," alisema.

Alisema sekta ya rasilimali watu ina mchango mkubwa kuiwezesha nchi kufikia malengo ya maendeleo ambayo imejiwekea na maendeleo endelevu yanayotekelezwa kwenye nchi husika.

Majaliwa alisisitiza mameneja hao kuhakikisha wanasimamia rasilimali watu ili kutoa thamani na tija kwa watumishi wa umma.

Alisema kwenye nchi kama rasilimali haziwezi kutekeleza wajibu kwa wananchi ni rahisi kuihukumu serikali kuwa haiwajibiki.

"Hivyo katika mkutano huu nawaomba tuwe wawazi katika kujadili changamoto na kujitathmini wenyewe fursa zilizopo katika utumishi wenu ili mkitoka hapa mkawe mabalozi wa utumishi wa umma kwa kuimarisha mifumo bora ya rasilimali watu na mkatoe mwelekeo katika taasisi zenu," alisema Majaliwa na kuongeza kuwa:

"Sekta ya umma yoyote lazima itambue umuhimu wa rasilimali watu sababu yenyewe ndio uti wa mgongo wa taasisi zote na hapo lazima kutekeleza majukumu yenu kwa weledi, uaminifu na juhudi ili kuleta maendeleo ya kiuchumi katika nchi zetu."

Pia aliagiza maofisa rasilimali watu wanaporejea kwenye nchi zao wakajengee uwezo viongozi ili kuendana na mabadiliko ya mara kwa mara, kuwakumbusha mwenendo na kanuni za kuwatumikia wananchi wao.

Vilevile, aliwaagiza kuongeza maono ya ubunifu na uadilifu katika kazi zao, kuongeza tija kwa upatikanaji na uendelezaji wa vipaji ili nchi ipate mafanikio, kuendeleza vipaji na nchi kupata mafanikio.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema mkutano huo ni muhimu, kwani unafanyika katika wakati ambapo dunia ina changamoto nyingi.

Simbachawene, alisema mijadala na mawazo ni muhimu kwa watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao.

Alisema ubunifu ni muhimu ili kuwezesha Bara la Afrika kukua zaidi katika teknolojia na rasilimali watu kuongezeka na kufanya kazi kwa tija.

Rais wa APS-HRMNet, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, alisema katika mkutano huo, washiriki watapata fursa ya kubadilishana uzoefu na utaalamu kwa lengo la kuwezesha nchi hizo za Afrika kupiga hatua katika maendeleo kwa kutumia mbinu za kisasa.

Alisema mtandao huo unaundwa na wanachama kutoka Afrika ambao wamegawanyika katika kanda tano, Afrika Magharibi nchi 17, Mashariki 10, Kati nane, Kaskazini sita na Kusini 13.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Msafiri Mbilu (wa pili kushoto), akisubiri kupokea maandamano ya watoto 39 waliopata kipaimara katika Usharika wa Muheza, mkoani Tanga juzi. Wengine ni Mkuu wa KKKT Jimbo la Tambalale, Mchungaji John Ndimbo (wa tatu kushoto) na (wa tatu kulia) ni Katibu Mkuu Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Julius Madiga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Watalii wamiminika Mkomazi

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

IDADI ya watalii wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro imeongezeka hadi kufikia 9,000 katika kipindi cha mwaka mmoja na kuiingizia serikali mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, wakati akizindua msimu wa pili wa tamasha la utalii la 'Same Utalii Festival' litakalofanyika kati ya Desemba 20 hadi 22, mwaka huu.

Alisema kuwa idadi hiyo imeongezeka kutoa watalii 7,000 waliotembelea katika hifadhi hiyo katika kipindi cha msimu msimu wa mwaka juzi.

"Tulifanya tamasha la kwanza mwezi Februari mwaka huu kutokana na umuhimu wake na mwamko mkubwa wa wananchi na wadau wa utalii.

"Tumekubaliana kuwa tamasha hili litakuwa likifanyika Desemba kila mwaka; mwaka huu litawajumuisha watu 20,000," alisema Kasilida.

Alisema wameamua kufanya tamasha hilo kwa mara ya pili mwaka huu kutokana na kuwapo kwa maombi mengi ya wadau wa utalii kutoka ndani na nje ya nchi, ambao wanafurahishwa na vivutio vilivyoko kwenye hifadhi hiyo, wakiwamo Faru.

Alisema uzinduzi rasmi wa tamasha hilo utafanyika Desemba 20, mwaka huu na kwamba kutakuwa na maonesho ya bidhaa za utalii, utamaduni na taasisi.

Kasilida, alisema baada ya uzinduzi kukamilika, watu na wageni watapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii, ikiwemo kilele cha Mlima Shengena uliopo Msitu wa Hifadhi wa Chome (CNFR) unaozungukwa na vijiji 27.


Alisema asubuhi ya tarehe 21 kutakuwa na mbio za Marathon zenye umbali wa kilomita tano, 10 na 21, wananchi na wadau waliojisajili mapema watashiriki.

"Kwenye tamasha hilo kutakuwa na matukio ya utangulizi kabla ya kufika tarehe 20 ya kuanza, tukio la kwanza ni utalii wa afya, watu watapata fursa ya kupima afya zao na kupata matibabu kutoka kwa madaktari ambao watakuwa wameandaliwa kuanzia tarehe 17 hadi 19," alisema Kasilda.

Alilitaja tukio jingine kuwa ni utalii wa usafiri wa gari moshi kutoka jijini Dar es Salaam hadi Same, kutakuwa na mabehewa manne ambayo yatakuwa na burudani, ikiwamo muziki.

Kasilda, ametaja utalii mwingine ni wa nyama choma kwenye mabehewa hayo, vinywaji na michezo.

Mmoja wa wadau wa utalii wilayani hapa, Halfan Peter, alisema hiyo ni fursa kwao katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka kutokana wananchi kujitokeza kwenye tamasha hilo kujionea vivutio.



# Wazee wakosa matibabu bure, kisa 70,000/-

**Na Timothy Itembe,** RORYA

BAADHI ya wazee wilayani hapa Mkoa wa Mara wamedai maisha yao yako hatarini kwa kukosa Sh. 70,000 kwa ajili ya kupata msamaha wa matibabu katika ofisi ya halmashauri.

Madai hayo yametolewa licha ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 kuelekeza wazee, wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupata huduma za matibabu bure kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya vya serikali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na mwandishi wa habari hizo, wazee walidai kuwa wamekata tamaa kupata huduma hiyo inayotolewa na serikali kwa kukosa kiasi hicho cha fedha.

Walidai pamoja na kukosa fedha hizo kupata barua hizo, wako hatarini kufa kwa kushindwa kugharamia matibabu.

Mmoja wa wazee hao, Thomas Patrick, Mkazi wa Kijiji cha Ruhu wilayani hapa alidai kuwa wanakabiliwa na usumbufu mkubwa wanapohitaji matibabu na kuitaka serikali kuboresha huduma kwa rika lao ili kunusuru maisha yao.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Dk. Khalfanis Eloleonlya, alithibitisha wazee hao kukosa huduma hiyo kutokana na uhaba wa vifaa tiba na dawa katika maeneo ya umma ya kutolea huduma za afya.

Eloleonlya, alisema halmashauri hiyo ina lengo la kuwajumuisha wazee 7,666 wilayani hapa katika mfumo wa usajili wa kupata huduma za matibabu bure.

Hata hivyo, alisema bila kuwapo kwa vifaa tiba na dawa, sera hiyo ya matibabu bure kwa rika hilo, itakuwa vigumu kutekelezeka.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Alphan Haule, alionesha kushtushwa na taarifa za wazee kwa kutumia gharama kubwa kupata huduma za matibabu licha ya kuwa katika mpango wa serikali wa kupata matibabu bure.

Haule, aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo kutekeleza wajibu wao ili makundi yaliyoko katika mpango huo wa serikali yapate huduma bure.

Alisisitiza umuhimu wa haki za wazee kupata huduma za afya bure katika hospitali, zahanati na vituo vya afya vya serikali.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uchaguzi wa serikali za mitaa wa Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Lango maziwa makuu lakithiri kwa ujambazi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI na wafanyabiashara wa Kata ya Busoka, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamechanga zaidi ya Sh.milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi kutokana na kukithiri kwa unyang'anyi wa kutumia silaha na mauaji katika eneo hilo lango la nchi za Maziwa Makuu.

Wakizungumza juzi wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi wa kituo hicho, baadhi ya wakazi hao, akiwamo mwenyekiti wa wafanyabiashara wa kata hiyo, Maulid Kwilasa alisema kuwa Oktoba 5, mwaka jana, wakala wa fedha za mitandao, alivamiwa na majambazi wenye silaha, kumjeruhi kwa kumpiga risasi kisha kumpora fedha.

Kwilasa, alisema mwaka huu, majambazi walivamia Kituo cha Mafuta cha Karagwe kilichoko katika eneo hilo na kupora fedha zote za mauzo.

Kwilasa, alisema uvamizi unaofanywa na majambazi na wezi, umesababisha baadhi ya wakazi na wafanyabiashara kuhama eneo hilo kwa kuhofia kuuawa.

"Eneo hili ndio lango la kuingia na kutokea kuelekea nchi za maziwa makuu, tunaiomba serikali ituunge mkono kukamilisha kituo hiki ili tukabiliane na majambazi na wezi," alisema.

Diwani wa Kata hiyo, Julius Malale alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 1.6 zimechangwa na wananchi kupitia jamii 24 kwa kila moja Sh.70,000, wafanyabiashara Sh. milioni moja na nyingine wadau akiwamo Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba.

Malale, alisema kata hiyo inahitaji kuwa na kituo hicho kwa sababu ni lango la kuingia na kutokea wahamiaji kutoka nchi hizo za maziwa makuu za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Lameck Evarist, alisema Ofisi ya Mkurugenzi kwa kutambua umuhimu wa ulinzi na usalama wa wananchi, imechangia mafuko 40 ya saruji na kamati ya maendeleo ya kata tofari 1,000 kufanikisha ujenzi huo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mboni Mhita, aliwashukuru wananchi na wafanyabiashara hao kwa kuisaidia serikali, hivyo anaungana nao kwa kuchanga Sh.milioni moja.

Mboni, aliahidi kuweka samani baada ya ujenzi wa kituo hicho kukamilika na kuwahimiza wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuwafichua wahalifu mitaani.

# Meya aikomalia TARURA barabara ya dampo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MEYA wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko ametoa wiki moja kwa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani hapa kukarabati haraka iwezekanavyo barabara kwenda dampo.

Masumbuko alitoa amri hiyo juzi kwenye kikao cha baraza la madiwani la manispaa hiyo wakati akijibu hoja ya Diwani wa Kata ya Kizumbi, Reuben Kitinya, lilipo dampo hilo kutokana na barabara hiyo kuharibika vibaya.

"TARURA mnapaswa kuchukua hatua haraka kuifanyia ukarabati barabara ya huko Kizumbi, na ninatoa wiki moja na nipate mrejesho hatuwezi kila siku linalalamikiwa jambo hilo hilo na hakuna utekelezaji," alisema.

Diwani Kitinya, awali akitoa malalamiko kuhusu ubovu wa barabara hiyo, alisema ina mabonde mengi na kusababisha magari ya kusomba taka kukwama.

Mhandisi wa TARURA wa Wilaya ya Shinyanga, Kulwa Maige, akizungumza kwa niaba ya meneja wa wakala huyo kwenye kikao hicho, alisema maagizo hayo wameyapokea na kuahidi kuyafikisha kwa mkubwa wake ili yafanyiwe kazi.

# Watendaji wakabidhiwa pikipiki kwa kuonywa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, David Rwazo, amewataka watendaji wa kata kutumia pikipiki katika utekelezaji majukumu yao.

Rwazo, alitoa rai hiyo juzi wakati akikabidhi pikipiki hizo kwa watendaji hao, Joyce Mahina (Lyamidati), Majahasi Jackson (Lyabusalu) na Mary Shausi (Tinde), kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Kalekwa Kasanga.

Alisema lengo la kuwakabidhi pikipiki hizo ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi za serikali, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ukusanyaji mapato kwenye kata zao.

Aliwaonya kutumia pikipiki hizo kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kugeuza mradi wa kujiingizia kipato kwa biashara ya bodaboda.

Watendaji hao, waliishukuru serikali kwa kuwapatia vitendea kazi hivyo na kuahidi kuzitumia pikipiki hizo kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kufanya kazi za serikali ili kuongeza ufanisi na kuwatumikia wananchi.





Ukurasa 12

Rose Njiro mpigania haki, ukombozi wa mwanamke kwenye jamii za Kimaasai




Ukurasa 13

## Ni siku ya uamuzi kwa wapigakura Marekani, vita Kamala Vs Trump kuingia White House

siasa

JUMATANO NOVEMBA 6, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Viongozi wajao serikali za mitaa wawajibike kwa wananchi ipasavyo

**Na Mwandishi Wetu**

ZIMEBAKI wiki tatu kufikia Jumatano Novemba 27 siku ya uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, jukumu linalofanywa kwa mujibu wa katiba ya Tanzania na sheria namba 287 ya halmashauri wilayani na 288 kwa halmashauri za miji na majiji.

Sina wasiwasi TAMISEMI kusimamia uchaguzi hata kama ni wizara ndani ya CCM, sheria zipo kukijitokeza 'dukuduku' wahusika waende mahakamani ili haki itendeke, kwa misingi ya sheria.

Tanzania yapo makabila zaidi ya 120 hivyo mitazamo au fikira tofauti kuhusu uchaguzi, usimamizi wake kadhalika, harakati zinakuwa nyingi hasa ikizingatiwa wingi wa vyama vya siasa ambavyo kisheria vinapaswa kuteua wagombea watakaochaguliwa kuongoza serikali za mitaa.

Kwa muktadha huo, malalamiko yanakuwa mengi, kutokana na fursa zilizopo mbele ya vyama vingi na wagombea husika. Nitoe rai kuwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 27, uwe wa mfano, Afrika na duniani kwa kuwezesha kupata viongozi mahiri na wenye maadili mema, wenye uchungu wa kuwaletea maendeleo wananchi na taifa kiujumla.

Kupitia viongozi watakaopewa fursa kuongoza serikali za vijiji na vitongoji ikiwamo wenyeviti wa mitaa kwenye manispaa na jiji. Mifumo, iliyopo ya kiutawala iwawezeshe Watanzania kuwa na matumaini ya kuharakishiwa mwendokasi upatikanaji maendeleo vijijini na kwenye mitaa mbalimbali mijini.

Kimsingi wengi ikiwamo viongozi kisiasa, watunga sera, wafanya maamuzi na watawala serikalini, tunaishi maeneo zilipo serikali za mitaa. Wilayani, manispaa au kwenye majiji kama Dodoma, Dar-es-Salaam.



Maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaofanyika mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

Kadhalika, ardhi imesambaa ziliko serikali za mitaa ikiwamo kila aina ya rasilimali zinazohitajika kwa maendeleo yetu. Mfano, chemchemu za maji, mito, mabwawa, maziwa, ardhioevu na kilomita zaidi ya 1,000 ukanda wa bahari kutoka Mtwara hadi Msumbiji, kisha Tanga mpaka Kenya.

Kwenye maeneo ziliko serikali za mitaa pia kunapatikana madini, vito vya thamani mbalimbali; misitu, mbuga, mapori ya akiba na tengefu yenye wanyamapori wengi. Vilevile, vijiji viko wilayani na baadhi kwenye maeneo ya miji na majiji ambako Watanzania wanaishi.

Tathmini nyingine inaashiria kuwa Watanzania walio wengi wanahitaji maendeleo ya uhakika, mathalani, huduma za kijamii zilizoboreshwa na kuimarika katika vijiji, kwenye vitongoji na mitaani sehemu za mijini, manispaa na majiji.

Hata hivyo, siyo kwamba tangu kupata uhuru hakuna maendeleo yapo lakini hayalingani na miaka 63 tangu wakoloni waondoke Desemba 9, 1961. Bado hali siyo bora hasa kwenye vijiji na katika mitaa mingi mijijini na majiji.

Huduma za barabara ni duni, maeneo ya makazi hayana mipangilio mizuri, nyumba zinajengwa bila utaratibu wenye taswira ya mipango miji. Ni changamoto kubwa kupata huduma kama za kiafya hususani kufikisha wagonjwa, wajawazito vituo vya afya hospitali pamoja na kuondoa takangumu. Vilevile, mifumo majitaka ni duni hivyo kutiririka hovyo mitaani.

Nimekuwa nikijiuliza Tanzania tunakwama wapi kujiletea maendeleo? Hakuna wataalamu wa fani mbalimbali kuwezesha wananchi, kusonga mbele kimaendeleo? Iwapo rasilimali tunazo mathalani, nguvukazi ipo ardhi ya kutosha nini hasa visababishi?

Je, ni siasa, sera, mifumo au sheria, kiutawala au kutokuwa makini au tunakosa maarifa? Naamini shughuli za kuwaletea maendeleo Watanzania zinahitajika wananchi wanakoishi, katika vijiji, vitongoji na mitaa mijini ambako kimsingi ndiko viongozi mahiri wa serikali za mitaa wanahitajika:

Wenyeviti wa vijiji, vitongoji, wajumbe wa mitaa ambao watapatikana baada ya uchaguzi utakaofanyika nchi nzima Novemba 27, 2024. Kwa uzoefu tulionao, na kwa kuzingatia malalamiko, mitazamo kuhusu kero mbalimbali za wananchi, inaelekea chaguzi katika serikali za mitaa, hatutilii mkazo sana kama ilivyo mkuu wa madiwani, wabunge, rais na makamu wake.

Inawezekana, kwa kujua au kutokujua, tukajikuta tunakosa werevu mzuri kuwapata viongozi wenye uwezo wa kuongoza na kusimamia maendeleo vijijini, kwenye vitongoji na mitaa mijini.

Ukiwasikiliza viongozi walio madarakani mathalani, kwenye mitaa baadhi wamekuwa walewale bila mabadiliko kwa muda mrefu.

Ukimuuliza Mtanzania unayomwona anafaa kuwa kiongozi mahiri katika mtaa, iwapo anaweza kugombea, anakataa.

Sababu huenda huko hakuna mvuto au motisha kama ilivyo kwa ubunge. Kadhalika, mahala viongozi wanapofanyia kazi ofisi za mitaa ni duni, ukilinganisha na umuhimu wake kwa kuzingatia ndiko huduma za msingi kwa wananchi zinakoanzia.

Baadhi wanaona ni kama kufanya kazi bila malengo halisi na hawawezeshwi inavyostahili kutimiza majukumu ipasavyo.

INAENDELEA UK. 13

# Simulizi ya Rose Njiro mpigania haki, ukombozi na heshima kwa mwanamke kwenye jamii ya Kimaasai

**Na Elizabeth Zaya**

WIKI iliyopita shujaa Rose, anaelezea alivyowaingiza mabinti shuleni, mbinu alizotumia kufikia mafanikio na leo anabainisha alivyogombea uongozi kisiasa...

Rose Njiro (40) anasema katika kuonyesha kwamba mwanamke anaweza na kuweka msisitizo kwamba mila kandamizi walizokuwa wanazishikilia Wamaasai kumwona hafai, hawezi na ni laana, aliwaonyesha kuwa hawakuwa sahihi.

Anajitosa kugombea ubunge mwaka 2021 katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Ngorongoro baada ya mbunge aliyechaguliwa kufariki.

Anasema alikuwa mwanamke pekee kati ya wanaume 16 waliojitokeza kuomba ridhaa ya CCM, kuteuliwa kupeperusha bendera ya chama.

"Nilitaka kuonyesha kuwa binadamu wote ni sawa na wana uwezo sawa, kwa sababu haijawahi kutokea mwanamke wa Kimaasai akagombea uongozi kwenye kitongoji au uongozi wa kimila. Walionekana ni laana kufanya hivyo, na hata historia ilikuwa inaonyesha kuwa tangu jimbo la Ngorongoro lianzishwe mwanamke hajawahi kugombea ubunge au kupatikana kiongozi wa kike iwe ni Mmasai au asiye wa jamii hiyo."

"Ule uthubutu uliwafungulia njia wanawake wengine katika jamii yetu hasa kwenye vyama vya siasa huku kuna wengine wameanza kugombea na wamechaguliwa. Lakini ningepewa nafasi ingekuwa fursa nzuri kwangu kuitumia kutafuta majibu ya migogoro ya ardhi ambayo imedumu kwa miaka mingi."

Anasema shida kubwa inayochangia hiyo ni kukosekana kwa mahusiano mazuri kati ya wananchi na serikali ndiyo maana haiishi, wakipatikana viongozi migogoro inazidi mpaka miaka mitano inaisha na hakuna maendeleo.

"Wilaya ya Ngorongoro kuna wawekezaji wengi, kuna fursa kubwa ya maendeleo, lakini kumekosekana mtu sahihi wa kuunganisha ili wananchi waachane na migogoro ya kila badala yake watumie fursa hizo kujiletea maendeleo," anasema Rose.

Anasema katika kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwaka kesho, tayari ameunda vikundi vya kuelimisha wanawake namna ya kusimama kugombea.

"Na nimewaambia waitumie vizuri hii fursa ambayo kwa sasa jamii imeamini uwezo wa mwanamke, wajitokeze kwa wingi wagombee kwa sababu uwezo wetu wanawake umetambulika na jamii yetu," anasema.



Rose Njilo (mwenye miwani), akijadili jambo na baadhi ya wasichana waliokimbia kuozwa, wanaoishi kwenye kituo chake kilichoko Moshono, mkoani Arusha. Kulia ni mwandishi, Elizabeth Zaya. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

> Tunachoshukuru ni kwamba mama anasali sana na sisi tunamuombea, tunaamini Mungu anamlinda hakuna wa kumdhuru.

## KUGOMBEA JIMBO

Rose anasema katika uchaguzi mkuu ujao amejipanga kugombea tena kwa mara ya pili katika jimbo la Ngorongoro akijinasibu kwamba kwa kazi ambazo amezifanya na kuonekana kwa jamii, ana uhakika wa kushinda kwa kishindo endapo chama chake cha CCM kitaridhia kumteua kuwania nafasi hiyo.

"Na sasa hivi napambana kwanza kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kuhakikisha kwenye nafasi hizo wanawake wengi wanaingia, kwa sababu ili nifanikiwe kule mbele lazima nihakikishe kwamba kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa tumefanya vizuri.

## KUSAIDIA WATOTO

Mbali na taasisi hiyo, Rose anasema mwaka jana alianzisha pia kituo cha kusaidia watoto wa kike wanaopitia ukatili wa kijinsia ikiwamo wale wanaokimbia kuozeshwa kwenye umri mdogo.

"Kwa hiyo tumetengeneza sehemu salama ambayo wanaishi, kama wanaendelea na shule wanatokea hapahapa kituoni, na wakati huo huo tunaendelea kutengeneza mahusiano na familia zao japo mahitaji yote tunawapatia sisi kituoni, pamoja na mambo mengine, tunawafundisha ufundi wa kushona, lakini wapo wanaosoma shule za msingi, na sekondari.

## MFANYAKAZI AZUNGUMZA

Mmoja wa wafanyakazi katika taasisi hiyo ya MWO, Saitoti Salingi, anasema Rose amefanya kazi ya kuleta mapinduzi katika maeneo mengi lakini kubwa ambayo imeleta matokeo mazuri na makubwa ni ya kufanya mapinduzi kwa jamii ya kimaasai kutoka kuamini mtoto wa kike ni laana hadi kufikia kuamini kwamba anaweza na kukubali kumpa nafasi ya uongozi katika jamii yao na kumruhusu kwenda kugombea kwenye chaguzi za kitaifa.

"Wakati anaanza kupambania hili, kila mmoja alimuona kama amechanganyikiwa wakisema tangu enzi za mababu na historia nzima ya jamii ya kimaasai haijawahi kutokea mwanamke akawa kiongozi sasa yeye anatawezaje, akapigwa vita kubwa si tu na viongozi wa mila kutoka ndani ya jamii yake lakini hata wale ambao wana nafasi za kisiasa kama madiwani, wenyeviti wa vijiji, lakini kwa Rose haikumyumbisha aliendelea mbele hadi alipohakikisha amevunja huo mwiko.

"Kuna wakati hata sisi tulikuwa tunaogopa na tunamshauri kwamba aachane nao tu maana ilikuwa ni hatari kwake, usalama ulikuwa ni mdogo lakini hakutusikiliza na baadae tulikuja kumwelewa nini alikuwa anaona mbele baada ya kuona haya mafanikio yaliopo kwa sasa katika jamii hii," anasema Salingi.

## HISIA ZA MTOTO WAKE

Kiranda Saning`o ni mtoto wa Rose, anasema wao wanafurahia kazi anayofanya mama yao licha ya kupitia misukosuko mingi lakini wanamuunga mkono.

"Tumeshuhudia maisha aliyopitia mama yetu wakati tunakua na mpaka sasa tumefikia hapa, ukweli kama una roho ndogo unaweza usikubaliane naye lakini sisi tunamuunga mkono kwa sababu akiacha yeye kufanya hakuna atakayefanya na wanawake wataendelea kuteseka katika jamii ya kimaasai," anasema Kiranda.

"Tunachoshukuru ni kwamba mama anasali sana na sisi tunamuombea, tunaamini Mungu anamlinda hakuna wa kumdhuru. Na kutokana na moyo wake huo wa kupambania watu wengine, ametuambukiza na sisi tunafanya hivyo, mfano mimi nikisikia kuna mtu yeyote ananyanyaswa hata ni shuleni huwa ni lazima nikaripoti na wakati mwingine namshirikisha mama."

## SAUTI YA DADAKE

Dada yake Rose, aliyejitambulisha kwa jina la Nayo Laang, anasema wakati ndugu yao huyo anapambania ukombozi wa mwanamke katika jamii hiyo, ilifika wakati wakawa wanatamani asiende tena kijijini kwao, kwa sababu wazee walikuwa wametangaza kwamba akionekana tu wanamuua kwa sababu anafundisha tabia mbaya wanawake.



Rose (kulia) na msichana anayefundishwa ushonaji kwenye kituo cha kusaidia wasichana waliokimbia ndoa za kulazimishwa. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

"Siku moja alipofika kijijini, mwenyekiti wa kijiji aliita watu wakakusanyika, halafu akawa ameshika sime, tukamuonyesha Rose ishara kwamba akimbie wanataka kumuua, lakini yeye alikataa, sasa wakati ndio Mwenyekiti anatoa sime ili ampige nayo, mimi nikakimbia kwenda kumkumbatia na hapohapo baadhi ya wanawake ambao tayari Rose alikuwa amewasaidia wakapiga kelele kwa nguvu, wakamkataza mwenyekiti asimpige.

"Walimwambia kama atampiga Rose kwa ile sime, wao watakwenda nyumbani kwake kumlaani, wakasema naye ni binadamu kama wengine na hakuna dhambi ambayo ameifanya na ana haki ya kwenda kijijini kwake kwa kuwa amezaliwa hapo, kwa hiyo zile kelele zilisaidia akaachiwa, lakini sisi kama ndugu tulikuwa tumeshakata tamaa kwamba wanamuua," anasema Nayo.

Nayo anasema wakati mdogo wao anapambana kuvunja mila hizo kandamizi, hata wao walikuwa wanaishi kwa wasiwasi na kuitwa majina mabaya lakini kwa sasa baada ya mapinduzi, wote wanatamani wawe karibu nao na wanataka waunganishwe wawe karibu na Rose.

## MWANAMKE KIONGOZI WA MILA

Kijoro Uyo ni miongoni mwa viongozi wa kimila wa kike waliochaguliwa mwaka huu, anasema licha ya Rose kupigwa vita, lakini ameonyesha ushujaa wa kupambana mpaka kuvunja 'kigingi' kilichowekwa enzi na enzi za mababu kwa jamii hiyo ya kimaasai na hata kufikia uamuzi wa kukubaliana naye kuingiza wanawake katika uongozi.

"Na mimi nilichaguliwa kuwa miongoni mwa viongozi hao sita wa kike ambao kwa sasa tunaingia kwenye vikao pamoja na viongozi wa kiume wa kimila na siyo kwamba tukiwa huko tunakaa kimya kama zamani, tunazungumza, wanatusikiliza na wanaamini hoja zetu nyingi tunazowaambia, kwangu mimi ni jambo kubwa sana," anasema Kijoro.

"Tena Rose ametuhamasisha tunasimama kugombea kwenye siasa, tangu ametuelimisha tunasimama wengi wanawake kugombea, na sasa hivi nimesimama kugombea kwenye nafasi ya uongozi na nimechaguliwa kuwa mwenyekiti wa UWT kijiji cha Moroni Tarafa ya Loliondo, na sasa hivi ametupa mwongozo wa namna wa kuhamasishana kusimama kwenye uchaguzi wa serikali zaa mtaa, na wengi sana wanawake wameonyesha nia ya kugombea, kwa kweli bila yeye(Rose) tungekuwa bado tumelala," anasema Kijoro.

Lengumo Parimilia, ni mmoja wa viongozi wa mila katika eneo hilo la Ngorongoro akitokea Kata ya Engarushorosamba, anasema wanamshukuru sana Rose kwa kusimama kwa nguvu kuwashawishi wakubali kuvunja mila waliyokuwa wanashikilia ya kutokuthamini na kumpatia nafasi mwanamke na kwamba tangu wakubaliane naye kuingiza wanawake katika jopo lao, wameanza kuona manufaa yake.

"Yaani muda mfupi tu baada ya kuwakubali wanawake kuingia kwenye uongozi tumeanza kuona manufaa yake, kwa miaka mingi sisi Malaigwanani wa eneo hili, hatukuwa na vitambulisho vya kututambulisha rasmi kwamba sisi ni viongozi, lakini sasa hivi Rose amepambana tumepewa na tumetambuliwa na serikali," anasema Parimilia.

"Si hilo tu, lakini sasa hivi tumeanza kuona maendeleo kwenye wilaya yetu, sasa tunaitwa mara kwa mara wilayani kwenye vikao vya maendeleo wakati zamani wala hatukuwa tunakwenda, na kila tukienda kwenye vikao hivyo, wanawake tulionao kwenye uongozi ndio wanasimama kupeleka hoja na tunaona zinakubaliwa kirahisi sana na ni wepesi sana kuzungumza na ni wakweli mpaka tunaona kwamba tulikosea sana kuwazuia zamani."

Parimilia anasema baada ya kuona matokeo mazuri na uwezo wa wanawake kwenye uongozi, sasa hivi wamewatangazia wananchi wote katika jamii yao kwamba hakuna kuwabagua tena wanawake katika jambo lolote na wametoa kibali rasmi kwa wanawake wote wanaotaka kugombea nafasi zozote za siasa wajitokeze na watachaguliwa kulingana na sera zao.

> Kwa hiyo tukasema mwanamke anayetaka uongozi kwenye vitongoji, udiwani au ubunge aende tu na hakuna wa kumtukana, atakayechaguliwa sawa na asiye chaguliwa sawa, washindane kwa uwezo wao.

Anasema zamani wanawake walikuwa wakijaribu hata kusimama kuzungumza katika jambo lolote kwenye vikao au mikutano ya hadhara, wanatukanwa lakini kwa sasa wamepiga marufuku hilo na kwamba yeyote atakayesimama na kuwatukana watamchukulia hatua kali.

"Tumeona hakuna tena sababu ya kuwazuia maana uwezo wao tumeuona, wanafanya vizuri sana. Na kupitia uwezo wao ambao tumeona kwa muda mfupi, tukasema kumbe ndio maana sasa hivi Rais ni Mwanamke na anafanya vizuri, Spika wa Bunge naye ni Mwanamke na anafanya vizuri, na kuna mwanamke yuko hapa Ngorongoro anaongoza Jeshi la Polisi naye anafanya vizuri sana,

"Kwa hiyo tukasema mwanamke anayetaka uongozi kwenye vitongoji, udiwani au ubunge aende tu na hakuna wa kumtukana, atakayechaguliwa sawa na asiye chaguliwa sawa, washindane kwa uwezo wao," anasema Parimilia.

## OFISA MAENDELEO JAMII

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ngorongoro, Daniel Bura, anasema kazi aliyofanya Rose na anayoendelea kufanya ni kubwa katika jamii na kwamba wao kama serikali wanaithamini kwa sababu inaisaidia serikali kuletea maendeleo wananchi wake.

"Kama mtu amepambana kuvunja mila ambayo ni kandamizi kwa watu wake na ambayo imewatesa miaka mingi, akatoa elimu ikaanza kubadilika licha ya kwamba ni aina ya jamii ambayo ina mifumo yake iliyoishikilia kwa nguvu, hilo ni jambo jema sana na tumeliona kwa Rose akifanikisha hilo.

"Pamoja na kwamba siyo rahisi kubadilika kwa haraka, lakini mpaka sasa amefanya kazi kubwa sana na inaonekana, kama ambavyo hakuna serikali inayopenda mwananchi wake ateseke, au aonewe, ametusaidia sana na tumeshirikiana naye sana katika kuhakikisha jamii ile inapata maendeleo na tunamtambua kwamba ni miongoni mwa watu wanaofanya vizuri sana kuleta maendeleo katika jamii yake," anasema Bura.

## TUZO ALIZOPATA

Rose anasema kupitia kazi ambazo amefanya amepata tuzo kadhaa ikiwamo kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, waandaaji wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro, Maendeleo ya Jamii mkoa wa Arusha pamoja na Ubalozi wa Ireland.

"Sijivunii kwa sababu bado naona kama sijafika, lakini mahali nilipo kwa sasa nimeona nimefika mbali, kwa sababu kwenye hii jamii wamefika mahali wakaamini uwezo wa mwanamke kwenye uongozi kama ilivyo kwa mwanamume, kwa hiyo sasa hivi mwanamke kusimama kugombea nafasi yoyote kwenye uongozi kwenye jamii ya kimasai na uongozi wa serikali siyo laana tena na hilo ndilo jambo nashukuru kila siku," anasema Rose.

# Ni siku ya uamuzi kwa wapigakura Marekani, vita Kamala Vs Trump kuingia White House




Makamu wa Rais Kamala Harris, alipokuwa kwenye mkutano wa kampeni huko Pittsburgh, Pennsylvania Jumatatu wiki hii.
**PICHA/HABARI: CNN**

**Na Mwandishi Wetu**

WAMAREKANI wameanza kupiga kura kumpata rais ajaye, au mrithi wa Joseph Bidden, aliyeingia madarakani 2020. Wagombea wakiwa ni Makamu wa Rais Kamala Harris wa Democrat na Rais wa zamani Donald Trump wa Republican.

Ni siku ya uamuzi kwa wapigakura katika vita vya vyama viwili kuingia White House au ikulu na pia udhibiti wa Bunge Kuu au Congress, hata kama matokeo yanaweza kuchukua siku au wiki kupatikana.

Kila mmoja kati ya wawili hao wanahitaji angalau kura 270 kutoka kwenye majimbo ya uchaguzi ili kushinda.

Majimbo ya uwanja wa vita ni Arizona, Georgia, Michigan, Nevada, North Carolina, Pennsylvania na Wisconsin, ndiyo yanatarajiwa kuwa muhimu kwenye njia ya kufikia ushindi.

Harris na Trump walilingana kwa kura tatu kila mmoja katika majimbo ya New Hampshire ya Dixville Notch.

Wagombea hao Kamala na Trump walifanya kampeni za mwisho katika majimbo ya uwanja wa vita jana usiku.

Harris alimaliza kampeni yake ya siku 107 huko Pennsylvania, wakati Trump alizungumza huko Michigan ambapo amemaliza kampeni zake tatu za urais.

Kamala Harris na Donald Trump waliwalenga wapigakura wahanga au kizazi kipya au Gen-Z walipokuwa wakifanya kampeni kabla ya uchaguzi, ambao wengi wao watapiga kura kwa mara ya kwanza leo.

Jarida la Columbia la Chuo Kikuu cha Columbia liligundua kuwa Gen Z ni zaidi ya wapigakura milioni 40, wakiwamo wapigakura wapya milioni nane.

Suala la ushawishi wa mitandao ya kijamii kwa wapigakura hawa hauwezi kupuuzwa, kulingana na Aidan Kohn-Murphy, mwanzilishi wa kundi la utetezi la Gen-Z for Change.

Anaiambia CNN kwamba TikTok imesaidia kuwafahamisha vijana wengi kuhusu wagombea urais na kampeni zao na kinachongojewa ni kura zao.

Masuala muhimu kwa wapigakura wachanga ni "mabadiliko ya hali ya hewa, haki ya uzazi, ghasia za bunduki na uungwaji mkono wa Biden kwa serikali ya Israel," Kohn-Murphy anasema.

Anasema kwamba vijana walipata habari kutoka TikTok katika "mfano wa rika-kwa-rika, ambayo inaongoza watu kuunga mkono wagombea zaidi.

Pia anabainisha kuwa wapigakura wengi wa mara ya kwanza au wachanga hawazifahamu kashfa za kisiasa za awali - kama vile mkanda wa Rais wa zamani Donald Trump "Access Hollywood" - kwenye rada zao, lakini mitandao ya kijamii iliwawezesha kujifunza zaidi kuhusu wagombea hao.

"Tulikuwa kati ya darasa la tano na la saba wakati kanda za Hollywood zilipotoka. Tumepata ganzi kwa maneno na vitendo vya kutisha vya Trump, hata hivyo haya ni mambo ambayo hatujasikia nadhani mtandao wa TikTok imetoa njia ya kuwakumbusha na kuwashtua vijana." Anasema.

**TRUMP AMTAJA ADUI**

Rais wa zamani, Donald Trump anabishana kuwa wakati wa mkutano wa mwisho wa kampeni yake kwamba mpinzani wake wa kweli kwenye uchaguzi huu si Makamu wa Rais Kamala Harris lakini ni "mfumo mbaya wa chama cha Democrat'

"Tutashinda mfumo mbovu wa Washington. Kwa sababu sishindani na Kamala, ninashindana na mfumo mbovu wa Democrat. Hawa ni watu waovu."

Anasema Trump wakati wa mkutano wake huko Michigan, ulioanza baada ya saa sita usiku.

Trump anarudia ahadi zake nyingi za kampeni, kama vile kutoza ushuru mkubwa na kukabiliana na uhamiaji haramu hasa kutoka Mexico.

Wakati huo huo, mwanamama bilionea wa Marekani, Oprah Winfrey, alipanda jukwaani katika mkutano wa mwisho wa Kamala Harris huko Philadelphia usiku wa Jumatatu pamoja na vijana 10, wote wapigakura kwa mara ya kwanza.

"Sera ambazo Kamala Harris anapendekeza kwa haki za uzazi za wanawake na usawa wa elimu ndizo zinazoniongoza kumpigia kura," mpiga kura mmoja anamwambia Oprah.

Mpigakura wa mara ya kwanza Gen Z, anasema ilikuwa muhimu kwake kama Mmarekani mwenye asili ya Afrika "kutumia haki yangu ya kupiga kura, ambayo mababu zangu walipigania sana."

## Viongozi wajao serikali za mitaa wawajibike kwa wananchi ipasavyo

**INATOKA UK. 11**

Kwa uchaguzi wa Novemba 27, mamlaka za kuteua wagombea kwa nafasi mbalimbali wateuliwe walio makini sana na wenye upeo wa kutosha kuyasukuma maendeleo mbele.

Ni wakati muafaka wa kuwapata viongozi wazalendo, wenye maono na mioyo ya kujituma, wanaopenda kuwajali wananchi na kushirikiana nao katika kutatua kero na wawe karibu na wanaowaongoza wakishauriana nao mara kwa mara siyo tu kujitokeza nyakati za uchanguzi lakini wakishapata nafasi ya kuongoza hawaonekani hadi uchaguzi mwingine.

Viongozi wa aina hiyo hawana uchungu wala nia ya kushirikiana na wananchi kutokomeza umaskini, ujinga na maradhi, maadui wakubwa tangu uhuru zaidi ya miaka 63 iliyopita.

Kwa kuzingatia sera ya kupeleka madaraka mikoani, wilayani, vijijini na katika mitaa, ifahamike kuwa Watanzania wanataka mabadiliko ya kweli, wayaone maendeleo kivitendo siyo kinadharia. Uzalendo ni kuweka maslahi ya taifa na watu kipaumbele kuliko kujali maslahi binafsi kwa kujilimbikizia mali kupindukia.

Wagombea wajiulize kwa miaka mitano ijayo nitafanya nini kijijini ili kuinua hali ya maisha kwa wananchi? Kadhalika kwenye mitaa wana mikakati endelevu na inayotekelezeka kuhakikisha miundombinu inaimarishwa ikiwepo huduma za kijamii zilizoboreshwa na kutatua kero mitaani?

Watanzania tujiulize je, tunaielewa vizuri dhamiri ya utawala wa serikali za mitaa au wengi wetu 'tupotupo' ili mradi tunaishi? Ni vizuri kutambua umuhimu wa serikali za mitaa vijijini pia mijini na majijini kwa nia njema ya kufikia maendeleo endelevu.

Ni kweli hatujafikia hali hiyo lakini ajenda ni kupunguza kama siyo kuondokana na kero zisizo za lazima kwa wananchi. Iwapo msisitizo katika mipango mikakati ni kuleta maendeleo kwa wananchi pia mkazo uwekwe kwenye kuimarisha utendaji bora katika serikali za mitaa ambako ndipo wananchi wanakoishi.

Iko haja ya kutathmini kwa kina mifumo ya kuwaletea maendeleo wananchi kama ni halisi au vipi? Kama Mtanzania anayetamani kuwaona raia wakiishi kwenye mazingira halisia kimaendeleo. Wahenga wetu walisema yaliyopita si ndwele tugange yajayo, kwa kumaanisha kuwa tusiangalie yaliyotutangulia bali tusonge mbele ipasavyo. Kwa mantiki hiyo, tujizatiti ipasavyo ili Novemba 27, 2024 baada ya uchaguzi tuweze kuwapata viongozi bora na siyo "boraviongozi." Tena kufanya kosa siyo kosa lakini kukosea ni pale unaporudia kosa kwa kujua au kutokujua.

Malalamiko yanajitokeza mara kwa mara hivyo wakati umefika yawe historia. Hivyo, baada ya uchaguzi tutarajie kuyaona mabadiliko makubwa kiutendaji.



## HABARI DODOMA

## RC abeba kero za wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amefanya ziara ya ukaguzi miradi na kusikiliza kero za wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Kata ya Rungwa, Kalangali, Mwamagembe na Mitundu.

Hayo yamejumuisha ukaguzi wa miradi ikiwamo ukaguzi wa zahanati mpya ya Itumba, nyumba za watumishi, mradi wa ujenzi wa sekondari mpya ya Kalangali.

Miongoni mwa kero zilizowasilishwa na wananchi ni uchache wa watumishi na vitendea kazi shuleni na katika taasisi za afya, uhitaji wa umeme na maji, barabara, mbolea na mbegu za ruzuku.

Vilevile malipo ya wakati kwa watumishi na usikivu wa redio katika maeneo hayo yenye usikivu hafifu.

Akizungumza na wananchi, Dendego ameahidi kutatua kero hizo ikiwamo ya umeme na kuagiza utekelezaji wake ndani ya siku saba katika Kata ya Rungwa eneo la Sekondari.

Aliwaagiza maofisa ugani kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbegu, pembejeo, dawa za kuua wadudu na mbolea za ruzuku.

Dendego, aliwaagiza maofisa hao kuwashauri wakulima zaidi kujiandikisha katika daftari la pembejeo za kilimo ili waweze kufaidika na huduma hizo zenye gharama nafuu kwa kusambazwa na mawakala na vyama vya msingi.

Sambamba na hilo, mkuu huyo wa mkoa, ameagiza ujenzi wa Shule ya Sekondari Mpya ya Kalangali kukamilika sambamba na nyumba ya mtumishi na zahanati ya Itumba.

Charles Clement Mgama na Stephano Minja, wakazi wa Kata ya Rungwa, walieleza kufurahishwa na ujio wa mkuu huyo wa mkoa wilayani Itigi wakisema wana imani changamoto zao zinakwenda kupatiwa ufumbuzi.

" Ujio wa Mkuu wa Mkoa utaleta ufumbuzi katika changamoto zetu nyingi ikiwapo changamoto ya umeme, maji, barabara, migogoro ya ardhi na watumishi," alisema Mgama.

# Wakulima kuzalisha kwa tija kwa umeme wa jua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKULIMA wadogo zaidi ya 100 wa Kata ya Matumbulu jijini Dodoma, wamepewa mafunzo ya matumizi ya nishati ya umeme jua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza tija.

Mafunzo haya yameandaliwa na Taasisi ya African Centre for Media Excellence (ACME) ya nchini Uganda kwa lengo la kusaidia wakulima kuongeza tija kwenye mazao yao ya kilimo na kipato cha kujikimu na familia zao.

Zaidi ya asilimia 90 ya wakulima hao wamekuwa wakitegemea visima na mabwawa kwa kutumia pampu za mafuta dizeli na petroli kuvuta maji na kuathiri uzalishaji mazao kutokana na fedha nyingi kununua nishati hiyo.

Katika mafunzo hayo, wakulima hao wamepewa elimu ya namna ya kutumia umeme jua kwa gharama nafuu ikiwa ni mbadala wa mafuta.

Marry Mabwahi, mkulima wa nyanya na katika kata hiyo, alisema anatamani kutumia umeme jua kwenye kilimo chake, lakini changamoto kubwa ni gharama za vifaa.

"Ombi letu kama wakulima ni kupunguziwa gharama ili na sisi wa hali ya chini tuweze kutumia na kunufaika na kilimo chetu. Tunashukuru leo tumepewa wazo la kujiunga kwenye vikundi vya ushirika ambavyo vinaweza kutusaidia kupata mikopo ya kununua vifaa vya umeme jua ili kujikwamua na hali hii," alisema.

Melea Benjamin, mkulima wa zabibu, mahindi na nyanya, alisema amekuwa akitumia umeme jua kwa matumizi ya nyumbani, mafunzo hayo yatasaidia kuongeza tija kwenye kilimo na kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Kilimo wa Kata hiyo, Aneth Mnana, alisema katika eneo lake mwitikio wa wakulima kulima kwa kutumia umeme jua ni hafifu wengi wanalima kilimo cha kizamani cha kumwagilia kwa kutumia visima na mabwawa yanayoendeshwa kwa pampu zinazotumia mafuta ya dizeli na petroli.

Alisema baadhi ya wakulima walioanza kutumia umeme huo wameanza kuona faida hasa kwenye kilimo cha bustani cha mazao ya nyanya, vitunguu na pilipili mboga (hoho).

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi Don Bosco Dodoma, Dk. Justine Mlebyia, alisema chuo hicho kimejikita kuzalisha wataalamu wa umeme jua kwa ajili ya miradi ya kilimo.

"Tunalenga kuhamasisha vijana na wakulima wengine kuangalia kilimo kama fursa, na si adhabu kwani ni muhimu kutumia umeme jua kuongeza tija katika maeneo yenye changamoto ya maji kama Dodoma," alisema Dk. Mlebyia.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akijadiliana jambo na Naibu wake, Dk. Doto Biteko, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwigulu asifu taasisi binafsi, benki kwa maendeleo nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali ina imani na sekta binafsi na taasisi za fedha kwa kuleta maendeleo na kukuza uchumi nchini.

Dk. Nchemba aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye hafla ya uzinduzi wa hatifungani ya Bondi Yangu inayoendeshwa na Benki ya Azania.

Alisema kwa kutambua mchanga wa sekta ya fedha katika maendeleo na kukuza uchumi, serikali imekuwa ikiweka juhudi kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya kisera na kisheria.

Alisema jitihada hizo ni kuwezesha ustawi wa sekta hiyo katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na benki, bima, masoko ya mitaji na dhamana na mifuko ya uwezeshaji.

Alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na wadau, wamekuja na mkakati wa kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Njia Mbadala (APF).

"Mkakati huu ukiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Mwaka 2020/21-2029/30 ambapo miongoni mwa malengo yake ni kuhakikisha taasisi zinatumia vyanzo bunifu na mbadala ambavyo vipo na vina uwezo wa kutoa mitaji," alisema Mwigulu.

Mkurugenzi wa Benki hiyo, Dk. Esther Mang'enya, alisema mwaka 2023 ulikuwa ni wa kwanza wa utekelezaji wa malengo ya mkakati na kufanikiwa kupata matokeo chanya.

"Tuliweza kukuza mizania kufika Shilingi trilioni 2.3 na kutengeneza faida ya Shilingi bilioni 29 na kuongeza gawio la Shilingi billioni 8.9," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi CPA, Felix Maagi, alisema katika kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa kifedha katika ujenzi wa uchumi wa taifa, benki hiyo imeanzisha akaunti maalumu.

"Akaunti hizo zipo kwenye makundi kama ya kinamama, vijana, wastaafu na sekta ya biashara hasa makampuni madogo madogo hasa kwa kuweka akiba katika kukuza biashara, " alisema.





# Wafugaji kuondolewa kwa nguvu Ihefu

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WAFUGAJI waliovamia Bonde la Ihefu lililoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani hapa Mkoa wa Mbeya, wameamriwa kuonda mifugo kabla ya operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu na kukamata kuanza.

Amri hiyo ilitolewa juzi na maofisa wa hifadhi hiyo na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mbarali kwenye kikao kilichowashirikisha viongozi wa mila, machifu, watemi na maleigwanani.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili namna ya kuondoa mifugo iliyoingizwa kwenye bonde hilo na kulinda ikolojia ya hifadhi hiyo na vyanzo vya maji ya Mto Ruaha Mkuu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme.

Mkuu wa Hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, alisema tatizo limeanza kuwa kubwa kutokana na baadhi ya wafugaji kutoka mikoa jirani kuanza kuingiza mifugo kwa wingi wilayani hapa kinyemela.

Meing'ataki, alisema baadhi ya wafugaji wameingiza mifugo ndani ya bonde hilo hasa eneo oevu ambalo halifikiki kirahisi kwa askari wanaofanya doria kwa miguu na magari.

Alisema mifugo hiyo inaonekana kwa askari wanapofanya doria kwa kutumia ndege.

"Tumeamua kuondoka makao makuu yetu kuja huku kushughulikia jambo hili, nyie viongozi wa mila mnasikilizwa sana na watu wenu, waambieni waondoe mifugo kule hifadhini, tukiwakamata hatua zitaendelea kuchukuliwa ikiwamo kutaifisha mifugo," alisema.

Meing'ataki alisisitiza kuwa kikao hicho ni kati ya njia ambazo wameamua kuzitumia kutatua tatizo hilo kabla hawajaanza kutumia nguvu kuondoa mifugo hiyo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbarali, Frank Sichalwe, aliwataka viongozi hao wa mila kuwa walinzi wakuu wa hifadhi hiyo kwa kuwazuia wafugaji kuingiza mifugo na kuwapokea wafugaji kutoka mikoa mingine.

Sichalwe, aliwataka askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kusimamia sheria kuhakikisha wafugaji ndani ya hifadhi hiyo wanaondolewa haraka.

Aliwataka wafugaji wilayani hapa kupunguza mifugo kwa kuuza baadhi na kuwekeza fedha kwenye miradi mingine kiuchumi kutokana na Mbarali kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikilinganishwa na uwezo wa maeneo yaliyotengwa kuchungia.

Aliwataka kufuga kisasa ili kupata tija na kupunguza migogoro inayoibuka mara kwa mara kati yao na hifadhi.

Katibu wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Barick Julius, alisema wilaya hiyo ina eneo linalotosheleza mifugo 60,000 na si zaidi ya 200,000 iliyopo kwa sasa.

Julius, aliiomba serikali kuwasaidia kupata vitalu kwenye eneo la Ranchi ya Taifa (NARCO) badala ya kutumia kwa kilimo.

Mmoja wa wazee wa mila, Julius Tisho, aliiomba serikali kutumia nguvu kuwaondoa wafugaji walioingiza mifugo ndani ya hifadhi hiyo ili kulipa ikolojia.

## Walimu wakuu wanolewa

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WAKALA wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) umetoa mafunzo kwa walimu wakuu wa shule za msingi zaidi ya 800 mkoani Ruvuma ili kuboresha utendaji kazi wao na kuinua kiwango cha taaluma kwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, mtendaji mkuu wa wakala wa ADEM, Dk. Maulid Jumanne Maulid, alisema wameendesha mafunzo katika halmashauri za mkoani humo kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 1, mwaka huu.

Dk. Maulid, alisema wakuu hao 814 wa shule hizo za serikali wamepata mafunzo hayo na ushiriki wao umekuwa ni wa asilimia 100, hivyo wanastahili kupongezwa.

Mratibu wa Mafunzo, Wakala wa ADEM Kituo cha Mbeya, Asha Kamando, aliushukuru uongozi wa serikali na elimu wa mkoa huo kuruhusu wakuu hao kushiriki mafunzo hayo ya kuimarisha uongozi na usimamizi wa shule.

Asha, alifafanua kuwa timu ya wawezeshaji kutoka ADEM imejipanga kufanya maandalizi ya kutosha na kusheheni wawezeshaji mahiri.

Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Edith Mpinzile, alisema serikali inaendelea kuhakikisha miundombinu ya shule za misingi na sekondari mkoani hapa ina kuwa bora na imara.

Aliwahimiza wakuu hao kutunza miundombinu hiyo na kuipongeza serikali kuwezesha ujenzi shule zake nchini.



Mmoja wa viongozi wa mila wa kabila la Wamaasai wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, Julius Tisho, akitoa maoni yake kwenye kikao kazi cha kukabiliana na tatizo la uingizaji wa mifugo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kati ya viongozi hao na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mradi kuzalisha ajira 1,000 nchini

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

MRADI wa uchimbaji madini ya chuma wa Maganga Matitu uliopo wilayani hapa unatarajia kuanza Mei mwaka 2025 na kuzalisha ajira kwa wananchi zaidi ya 1,000 nchini.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa Fujian Hexingwang industry Tanzania. Co. Ltd, Xu Xingda katika hafla ya kutambulisha kampuni hiyo itakayotekeleza mradi huo iliyofanyika wilayani hapa.

Xingda, alisema kampuni hiyo ina mpango wa kuanzisha mgodi wa kuchimba chuma na kiwanda cha kuchenjua madini hayo katika eneo hilo.

Alisema mgodi na kiwanda hicho kwa unatarajia kuzalisha ajira rasmi 200 na zisizo rasmi 800 na kutoa kipaumbele kwa wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na Mkoa wa Njombe.

Alisema kiwanda hicho kinatarajia kitazalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vingine vinavyohitaji chuma kuzalisha bidhaa na kuondokana na matumizi ya chuma chakavu.

"Upatikanaji wa malighafi hii ya chuma utaisaidia serikali kupunguza gharama za uagizaji wa chuma ghafi nje ya nchi," alisema Xingda.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utaanza baada ya wananchi ambao wameupisha kwa kutoa maeneo yao kulipwa fidia zao.

Msimamizi wa mradi wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Mhandisi Wallu Kapaya, alisema mandalizi ya mwisho ya utekelezaji wa mradi huo yanaendelea vizuri, Mei mwakani utaanza rasmi.

Kapaya, alisema mradi huo unatarajia kuchimba chuma tani 1,000,000 kwa mwaka na kutumika malighafi kutengeneza bidhaa zinazotokana na madini hayo.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Judica Omary, alisema mradi huo unakwenda kubadilisha uchumi wa wilaya hiyo na Tanzania.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema ataendelea kusimamia miradi hiyo inayotekelezwa katika wilaya hiyo kwa manufaa ya wananchi.

Aliiomba serikali kutenga bajeti ya kutosha kukamilisha ujenzi wa barabara ya Njombe - Ludewa kurahisisha mawasiliano na utekelezaji miradi mikubwa ya Liganga, Mchuchuma na huo wa Maganga Matitu.

## Mabilioni yaboresha miundombinu TIA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 58 kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujisomea kwa kampasi sita za Taasisi ya Uhasibu nchini (TIA).

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TIA, Profesa Jehovaness Aikael, aliyasema hayo kwenye mahafali ya 12 ya taasisi hiyo Kampasi ya Mbeya.

Profesa Aikael, alisema katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na mjumbe wa bodi hiyo, Sixbert Qamdiye kuwa uboreshaji miundombinu hiyo unahusisha ujenzi wa majengo vyumba vya maktaba, maabara za kisasa za kompyuta, kumbi za mihadhara na miundombinu mingine.

"Uboreshaji huu wa miundombinu umesababisha ongezeko la udahili kwenye kampasi zetu zote na bodi itahakikisha inatimiza wajibu wake wa kumshauri Waziri wa Fedha kuhusu mpango mkakati wa maendeleo ya taasisi hii," alisema.

Aliwaasa wahitimu hao kuwa wabunifu na kuthubutu kama nguzo kuu ya kutafuta ajira na kujiajiri.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa Willium Pallangyo, alisema kampasi ya Mbeya ilipokea shilingi bilioni 3.3 kutoka serikalini na kutumika kwenye ujenzi wa miundombinu ya kisasa.

Aliitaja miundombinu hiyo ambayo imeanza kutumika kuwa ni maabara ya kisasa ya kompyuta yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 180, maktaba ya kisasa wanafunzi 168, ukumbi wa mihadhara wanafunzi 260 kwa wakati mmoja, ofisi na ukumbi wa mikutano.

Kuhusu mikopo ya elimu ya juu kwa kampasi hiyo, alisema idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka wanafunzi 1,323 mwaka 2023 hadi kufikia wanafunzi 1,490 mwaka huu.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wenzake, Anzawe Mgeni, alisema elimu waliyopata itawasaidia kujiajiri na kuajiriwa kwenye taasisi za serikali na binafsi nchini.

Mgeni, alisema taasisi hiyo imejikita katika utoaji wa mafunzo ya vitendo hasa ujasiriamali na kuwaandaa wahitimu wake kujiajiri badala ya kutegemea kuajiriwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisisitiza umuhimu wa TIA kuendelea kuibua ubunifu wa ujasiriamali kwa wanafunzi wake ili kukabiliana na tatizo la ajira nchini.

Malisa, aliwaasa wahitimu hao kutumia elimu waliyopata kupambana na umaskini kwa kutumia fursa zinatotolewa na Serikali ikiwemo mikopo isiyo na riba kuanzisha miradi.



## HABARI ZANZIBAR

# CCM: Wapemba si mateka wa upinzani

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimetamba kuwa wananchi kisiwani hapa si mateka wa upinzani baada ya kubadili mtazamo, fikra na kuacha kuushabikia kutokana na kuridhishwa na serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuwaletea maendeleo.

CCM kimeendelea kutamba kuwa Pemba ya miaka 1995 sio ya sasa na kuna kizazi kipya kinachotofautisha kati ya utendaji makini na propaganda hasi za kisiasa kisiwani hapa.

Kauli hizo zimetolewa na Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Idara ya Itikadi na Uenezi, wa chama hicho visiwani hapa, Khamis Mbeto Khamis.

Mbeto, alisisitiza kuwa Pemba ya leo sio ile ya watu kuburuzwa bali ni ya mtazamo mpya na fikra njema endelevu.

Alisema kuna mambo huenda kule nyuma yaliwakatisha tamaa baadhi ya wananchi kisiwani hapa na kwamba baada ya kuvutiwa na utendaji wa serikali ya awamu ya nane, inayoongozwa na Mwinyi, Pemba imeachana na mitazamo hasi.

"Wananchi wanakiri kulikuwa na wakati Pemba kama ilisahauliwa kimaendeleo. Hivi sasa inashirikishwa katika maendeleo. Kwa sasa huduma zilizoko Unguja utazipata ukiwa Pemba. Macho ya mtu hayadanganyi bali huona ukweli," alisema Mbeto.

Aliendelea kusema kuwa wananchi hao wameacha kushabikia upinzani na kuepuka siasa zilizowagombanisha na kuisha kwa chuki na hasama katika jamii.

"Kusikiliza hadithi na kudai Pemba imetengwa na SMZ (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar), madai hayo ni upuuzi mtupu. Au kusema Wapemba wamebaguliwa kwa kuwa hawakushiriki Mapinduzi ya Zanzibar ni simulizi zisizo na mashiko," alisema.

Katibu huyo mwenezi, alisema viongozi wa upinzani kwa muda mrefu hutumia siasa za ukabila, asili na nasaba kuigawa jamii huku wakijua kuwa matamshi hayo ni hatari kutolewa na kiongozi aliyekomaa kisiasa.

"Hakuna namna ya kumgombanisha Muunguja na Mpemba. Wote ni Wazanzibari. Mwarabu, Mhindi, Mzungu, Mswahili au Mchina aliyezaliwa Zanzibar wote raia wa Tanzania," alisema Mbeto.

## Zanzibar, China kuimarisha ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar (SMZ) imeahidi kuendeleza ushirikiano baina yake na China kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Ahadi hiyo ilitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah wakati akizungumza na Naibu Gavana wa Jimbo la Zhejiang, Yang Qingjiu na ujumbe wake ofisini kwake Vuga visiwani hapa.

Abdullah, alisema SMZ inathamini na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na China kuvisaidia visiwa vya Unguja na Pemba kwenye sekta ya afya, kilimo, elimu, habari na miradi ya kimkakati.

Aliishukuru serikali ya nchi hiyo kwa kuendelea kuisaidia Zanzibar kupitia nyanja mbalimbali, ikiwamo kupokea madaktari bingwa kusaidia kutoa huduma za tiba na ushauri kwa wagonjwa katika hospitali za visiwa hivyo.

Abdullah alitaja kipaumbele cha SMZ kuwa ni uchumi wa buluu ambao unajumuisha Sekta ya Utalii ambayo imekuwa ikichangia pato kubwa la taifa kutokana na ongezeko la wageni wanaotembelea Zanzibar.

Ameikaribisha China kuja kuwekeza Zanzibar na kuzitumia fursa zilizopo nchini ikiwamo uchumi huo wa buluu.

Kwa upande wake, Qingjiu, alisema wako Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya nchi hizo hasa katika miradi ya maendeleo.

Alisema China imekuwa ikishirikiana na SMZ katika sekta ya uchumi, utamaduni na elimu kwa kuwapatia baadhi ya wananchi ufadhili wa masomo ya muda mrefu na muda mfupi hasa katika kada ili kuwaongezea maarifa watumishi wa umma.

Alisema jimbo lao la ZHEJIANG limepiga hatua kubwa katika biashara hivyo kwa kushirikiana na SMZ wanawekea mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wa pande hizo.



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akikabidhi tuzo ya kuthamini mchango wa Benki ya Stanbic Tanzania kwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Manzi Rwegasira kwa ajili ya kuchangia kusaidia gharama za matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo na mishipa ya damu nchini, katika harambee iliyoandaliwa na JKCI na Heart Team Africa Foundation, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Benki hiyo, ilichangia Sh. milioni 80. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SUZA kuboresha miundombinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHUO cha Taifa Zanzibar (SUZA) kinatarajia kutumia shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wake.

Ni baada ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa majengo mawili chini ya Mradi wa HEET na Kampuni ya Mohammed Bilders wenye lengo la utekelezaji wa elimu ya juu visiwani hapa.

Makamu Mkuu wa Chuo cha hicho Profesa Mohamed Makame Haji, alisema hatua hiyo itasaidia kuboresha sekta ya elimu ya juu visiwani hapa.

Akizungumza jana katika hafla hiyo ya utiaji saini ofisini kwake Tunguu, Haji, alisema awali kazi hiyo iliandaliwa na Serikali ya Tanzania kwa lengo la kuzijengea uwezo taasisi za elimu ya juu kuwa na vyuo bora nchini.

Alifafanua kuwa serikali ilikuja na wazo hilo baada ya kubaini kuwapo kwa mapungufu ikiwamo kwa wahitimu ya elimu ya juu.

"Haya ni mageuzi makubwa yaliyokuja, hivyo yatapelekea kuinua elimu ya juu ili kuleta maendeleo," alisema.

Alisema miongoni mwa maendeleo hayo ni pamoja na kuwawezesha wataaluma wa ufundishaji wa vyuo kuwa na mbinu mbadala kuwanoa vijana ambao ndio tegemeo kwa taifa.

Haji, alisema ujenzi huo utasaidia kuweka mazingira mazuri ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kurahisisha mawasiliano ili kazi ya ufundishaji ifikiwe kama ilivyokusudiwa na kuchukua miezi 18 hadi kukamilika kwake.

Profesa Haji, alisema SUZA kiasi hicho cha Sh. milioni 20 kimegawanywa katika sekta mbalimbali, asilimia kubwa katika ujenzi wa miundombinu hiyo.

Alisema ujenzi huo pia utanufaisha vijana wengi waliopo nje kujenga maisha yao na uwezo wa kielimu na kuchangia taifa lao.

Mkandarasi wa ujenzi huo, Mohammed Bilders Nizar Lakhani, alisema wapo tayari kujenga mazingira mazuri ya kujifunzia kwa ajili ya vijana wa Zanzibar wanojiunga na chuo hicho.

Msanifu majengo, Lazaro Peter aliwataka wajenzi kuacha kutengeneza mazingira ambayo yatapelekea kukwama kwa ujenzi huo. Ujenzi huo umejumuisha majengo ya maabara na shule ya kilimo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIETHA JAMES MGATA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye index namba **S4031/0024** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Mlandege Mwaka 2015. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/41566/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA E MACHUNDA** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba **NO.S.4994/0027/2018** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EDEN VALLEY SECONDARY SCHOOL.** Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MWA/MAG//2336/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTIAN SIMON SARAKIKYA** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP** kidato cha sita, yenye index namba **S0857-0654** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LONGIDO SECONDARY. Mwaka 2024. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIG//238490/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERICK JOHN MCHEMBE** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba **S0534/0159** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST.ANTHONY'S SECONDARY SCHOOL MBAGALA.** Mwaka 2013. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU//241B1/2024**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**DAVID JOHN KIANGO** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0347/0615** iliyotolewa na **TAMBAZA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/236015/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MATHEW MUSYANGI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba **S.136/74** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MUSOMA SECONDARY SCHOOL** Mwaka 1981 Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **URP/IR/87**

## TANGAZO LA KAZI/UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya ualimu mchepuo wa kingereza kwa masomo yote na madarasa yote kuanzia chekechea Hadi darasa la saba, sifa za chekechea ni certicate au diploma na kwa darasa la kwanza Hadi la saba ni diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliano 0783298900**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**VALERIAN SEBASTIAN SHAYO**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI **T542BJL** CHASSIS NO **ZZE1222011060** ENGINE NO **tZZ1264836** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**PHQ/ARU/ARU/41301/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**MATHAYO FRANCIS MASELE**

Anatangaza kupotelewa na kadi za gari (Toyota cresta/Toyota vits) zenye namba za usajili **T 768 BHZ, T 819 DTH,** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/37710/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMSON OURO ONYAUGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MISTUBISH CANTER** yenye namba ya usajili **T999AAW.** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/DAR/KIN/232467/2024**

## KUPOTE KWA KADI ZA GARI

**ABDULRAHMAN AMOUR KHAMISI** anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye namba za usajili **T350 BNT, T277BRE, T106 BSG, T523BYZ, T969BZA, T467CJF, T312 CNB, T469 DGX** Yeyote atakae ziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/DAR/UBU/240798/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WEBBY MORRISS JULIUS** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T349AHG** aina ya Toyota Corolla, Chassis **No. AE1003056265,** Engine No 5A8557511. . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/49983/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LIBERTY SAMSON KALAMJI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya Toyo yenye namba ya usajili **MC845 ACG** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/SIM/BUS/4805/2024**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Mirathi Na. 1767 2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MALIKI OMARI HOZA wa DAR ES SALAAM**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA HOZA MALIKI OMARI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 11 Mwaka 2024 saa 1:30 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia**
1. Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa
2. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
3. Marehemu hakuacha wosia

**Futa isiyohusika**
Imetolewa leo Tarehe 09 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NAMBARI 17882 LA MWAKA 2024**
**(Asilia kesi ya Madai Nambari 07/2022 Mahakama ya Wilaya Kyela)**

**RELIAANCE INSURANCE COMAPANY TANZANIA LIMITED .... MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **FRANK PATSON**
2. **HAROLD JOHN KALUNGA**
3. **BEATUS STEPHEN KABAKA..........................WAJIBU MAOMBI**

**KWA:HAROLD JOHN KALUNGA**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI WA PILI**

Unataarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe 14/11/2024 siku ya Alhamisi saa 3:00 kamili asubuhi bila kukosa ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.

**ELEWA KWAMBA,** Ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi utatolewa.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 17/10/2024.

**NAIBI MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

---

**(Rule 13 Civil Procedure Sammons and pleading)**

**IN THE DISTRICT COURT OF MPANDA AT MPANDA**

**CIVIL APPEAL CASE NO 25137 2024**

**APPELLANT SAMSON MAHWAGO**

**VERSUS**

**SELEMANI JAMES AND TWO OTHERS MAIKO EDWIN REPONDENT TO MAIKO EDWIN**

**TAKE NOTICE** that the hearing of the above suit has been set down for 15 days of 11, 2024

You must product on that day all at the witnesses upon whose evidence and all the document upon which you intend so really in support of your case.
Given under my hand and the seal of this court this 25 Days of 10,2024

**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**MISC. PROBATE APPLICATION NO 21430 OF 2024**
**(Arising from the Ruling of the District Court of Dodoma at Dodoma in Probate and Administration Cause No. 144 of 2023 dated 02/02/2024)**
**In the Matter of the estate of the late FRISMILLER UPEMDO MSHANA Dodoma District**
**And**
**In the matter of application for revocation of letters of Administration and grant the same to the Applicants**
**Between**
**REHEMA MSHANA LUBUVA...............................1ST APPLICANT**
**ROSE LEONARD MSHANA..................................2 NDAPPLICANT**
**SALMA IDDI MSAFIRI.......................................3RD APPLICANT**
**VERSUS**
**ERICK LEONARD PIUS, the Administrator of Estate of the Late FRISMILLER UPEMDO MSHANA..........RESPONDENT**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named Applicants.
Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of 11...................... 2024
Dated at Dodoma this 28th day of 10......................2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**FORM 58**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**IN THE COURT DISTRICT DELEGATE OF ARUSHA DISTRICT AT ARUSHA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26823 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late DAVID SHIKURIAL MASAWE**

**And**

**In the Matter Application for Probate of the Will of the Late**
**BY MOSES DAVID MASSAWE & ROSEMARY DAVID MASSAWE**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they thick fit before the grant of probate is made to the above -named petitioner
Objections to the grant should be find on or before the 07th day of November 2024.
The Will of the said deceased is deposited and open for inspectional at the court.
**Dated at 28th day of OCTOBER 2024.**

**RESIDENT MAGISTRATE.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ni mtifuano wa Kamala, Trump kukalia kiti cha Ikulu Marekani

**Christina Mwakangale na mitandao**

LEO ni kinyang'anyiro cha kuwania urais Ikulu ya White House, mchuano mkali ukiwa kati ya Kamala Harris (60) na Donald Trump (78).

Mgombea wa Chama cha Democratic, Kamala Harris, Makamu wa Rais wa sasa na mgombea wa Chama cha Republican, Donald Trump, rais wa zamani wa Marekani, wana ushindani unaokaribiana sana.

Ushindi mwembamba unaweza kusababisha kura kuhesabiwa upya. Jimbo la Pennsylvania, kwa mfano, kuhesabiwa upya kwa jimbo zima kutahitajika, ikiwa kutakuwa na tofauti ya nusu ya asilimia kati ya kura zilizopigwa.

Hata hivyo, Jumuiya ya Kijasusi ya Marekani, imeitaja Russia kama tishio kubwa zaidi kwa uadilifu wa uchaguzi katika taarifa iliyotolewa juzi.

Taarifa hiyo kwa mujibu wa BBC Swahili, ilitiwa saini na Ofisi ya Mkurugenzi wa Ujasusi wa Kitaifa (ODNI), Ofisi ya Shirikisho ya Upelelezi (FBI) na Wakala wa Usalama wa Mtandao na Miundombinu (CISA).



Donald Trump



Kamala Harris

### KUVUNJA MWIKO WA MIAKA 130

Kutokana na ushindani unaokaribiana kati ya Trump na Kamala, kuna uwezekano wa historia ya rais aliyeshindwa, kuweza kuchaguliwa tena, kwa mara ya kwanza katika miaka 130.

Idadi ya waliopiga kura mapema nchini Marekani imepita milioni 81, kulingana na Chuo Kikuu cha Florida Election Lab, nchini humo.

Hadi mkesha wa kuamkia siku ya kupigakura (jana), watu 81,379,684, tayari walikuwa wameshapiga kura, 44,402,375 wakiwa wamefika katika vituo vya kupiga kura wenyewe, huku kura 36,977,311 zikiwa zimepigwa kama barua kupitia njia ya posta.

Hiyo ni sababu inayoweza kutajwa kwamba ni desturi za kupiga kura za raia wa Marekani, zimebadilika tangu kutokea kwa mlipuko wa Uviko-19.

Ingawa idadi ya wapigakura wa mapema mwaka huu, haitapita ile ya wakati wa janga la Uviko 19, imezidi ile jumla ya kura za mapema zilizopigwa mwaka wa 2016 (milioni 47.2) au 2012 (milioni 46.2).

### KINACHOMPAISHA TRUMP

Kwa mujibu wa ukurasa wa BBC, ushindi wa Trump umeganwanyika maeneo kadhaa. Mosi, Trump kutokuwa madarakani. Uchumi ni kipaumbele kwa wapigakura na wakati ukosefu wa ajira ni mdogo na kupanda kwa soko la Wamarekani wengi wanasema wanakabiliana na ongezeko la gharama za maisha.

Mfumuko wa bei ulifikia viwango ambavyo havijawahi kushuhudiwa tangu miaka ya 1970, baada ya janga la Uviko 19, ikimpa Trump nafasi ya kuhoji 'Je, hali ni bora sasa kuliko miaka minne iliyopita?'

Mwaka huu, wapigakura duniani kote wamevitupilia mbali vyama tawala kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, baada ya janga la Uviko 19. Wapigakura wa Marekani pia wana shauku ya mabadiliko.

Ni robo pekee ya Wamarekani, wanasema wanaridhishwa na uelekeo wa nchi, huku theluthi mbili wakishindwa kuridhishwa na hali ya uchumi.

Katika hili, Kamala amejaribu kuwa mgombea mpigania mabadiliko, lakini kama makamu wa rais amekuwa na kibarua kigumu cha kuonesha utofauti kati yake na Joe Biden, ambaye hakuwa mgombea maarufu.

Pili Trump hakabiliwi na shutuma nyingi. Licha ya msukosuko wa ghasia za Januari 6, 2021 katika Ikulu ya Marekani, mfululizo wa mashtaka na hatia ya jinai ambayo haijawahi kushuhudiwa, uungwaji mkono wa Trump umesalia thabiti kwa mwaka mzima kwa asilimia 40 au zaidi.

Wakati chama cha Democrats na wahafidhina wanaompinga Trump wanasema hafai kushika wadhifa huo, Warepublican wengi wanamuunga mkono, huku Trump akisema yeye ni mwathirika wa kisiasa.

Huku pande zote mbili zikiwa zimejizatiti, anahitaji tu kushinda kiasi cha kutosha cha wapigakura, ambao bado hawajaamua kura yao watampigia nani.

Tatu, Trumpa ana maonyo yake juu ya uhamiaji haramu na yanasikika. Kando na hali ya uchumi, uchaguzi mara nyingi huamuliwa na suala lenye mvuto wa kihisia.

Democrats wanaitegemea sera ya utoaji mimba, huku Trump akiweka dau kwenye uhamiaji.

Baada ya makabiliano ya mpakani kuvuka viwango vya rekodi chini ya Biden na idadi ya wahamiaji kuathiri majimbo ya mbali na mpaka.

Kura za maoni zinaonesha wapigakura wanamwamini zaidi Trump, kuhusu uhamiaji na kwamba anakubalika zaidi Amerika Kusini, kuliko chaguzi zilizopita.

Nne, kwa Trump wengi hawana shahada. Wito wa Trump kwa wapigakura wanaojiskia kusahaulika na kuachwa.

Hapo nyuma, umebadilisha siasa za Marekani kwa kugeuza majimbo ya asili ya Democrats, kama chama cha wafanyikazi kuwa Republican na kuimarisha ulinzi wa viwanda vya Marekani kwa kuwapo ushuru.

Jambo la tano, Trump anaonekana kama mtu mwenye nguvu katika dunia isiyo na utulivu. Wapinzani wa Trump wanasema anadhoofisha miungano ya Marekani, kwa kujihusisha na viongozi wa kimabavu.

Trumpa, rais huyo wa zamani anaona kutotabirika kwake kama uimara wake hata hivyo, anasema kwamba hakuna vita kubwa vilivyoanza alipokuwa katika Ikulu ya White House.

Wamarekani wengi wanakasirishwa, kwa sababu tofauti kama Marekani kutuma mabilioni ya pesa Ukraine na Israel na kufikiri Marekani ni dhaifu chini ya utawala wa Biden.

Wapigakura walio wengi hasa wanaume ambao Trump amekutana nao kupitia podikasti kama vile Joe Rogan, wanaona Trump kama kiongozi mwenye nguvu zaidi kuliko Harris.

### KINACHOMPAISHA KAMALA

Kamala, yeye sio Trump. Licha ya kunufaika kwa uwapo wa Trump. Anabaki kuwa mtu wa tofauti sana. Mwaka 2020, alishinda rekodi ya kura kwa mgombea wa Republican, lakini alishindwa kwa sababu Wamarekani milioni saba, zaidi walijitokeza kumuunga mkono Biden.

Wakati huu, Kamala anakabiliana na ujio wa Trump. Anamwita 'fashisti' na tishio kwa demokrasia. Kura ya maoni ya Reuters, Julai, mwaka huu, ilionesha kuwa Wamarekani wanne kati ya watano wanahisi nchi hiyo inazidi kudorora.

Kamala, anatarajii wapigakura haswa Republican wenye msimamo wa wastani watamuona kama mgombeaji mwenye utulivu.

Pili, Kamala sio Biden. Democrats walikuwa na kila uelekeo wa kushindwa Biden, alijiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho. Wakiwa wameungana kwa shauku ya kumshinda Trump, chama hicho kilimuunga mkono Kamala haraka, huku akiungwa mkono tangu alipotia nia, alitoa ujumbe wa kusonga mbele bele zaidi ambao ulisisimua.

Pia, Kamala, amepunguza baadhi ya zilizokuwa sera za Biden. Mojawapo ni umri. Kura za maoni mara kwa mara zilionesha kwamba, wapigakura walikuwa na wasiwasi juu ya Biden kufaa kushika nafasi ya urais.

Sasa kinyang'anyiro kimebadilika na ni Trump ambaye anawania akiwa mzee zaidi kuwahi kushinda Ikulu ya White House.

Tatu, Kamala, amepigania haki za wanawake. Huu ni uchaguzi wa kwanza wa rais tangu Mahakama ya Juu ya Marekani, kubatilisha Roe v Wade na haki ya kikatiba ya kutoa mimba.

Wapigakura wanaounga mkono kuhusu kulinda haki za uaviaji mimba kwa wingi walimuunga mkono Kamala. Katika chaguzi zilizopita, hasa mihula ya kati ya 2022 suala hilo linaweza kuchochea watu kujitokeza kupiga kura na kuathiri

### MATOKEO JE?

Wakati huu, majimbo 10, ikiwa ni pamoja na jimbo la swing Arizona, yatakuwa na mipango ya kupiga kura kuwauliza wapigakura, jinsi utoaji mimba unapaswa kudhibitiwa. Hii inaweza kuongeza uungwaji mkono kwa Kamala.

Nne, Kamala, wapigakura wake wanauwezekano mkubwa wa kujitokeza. Makundi ambayo Kamala, anaungwa mkono mkubwa, kama wasomi wa chuo kikuu na wazee, wana uwezekano mkubwa wa kumpigia kura.

Trump, kwa mfano, anaongoza miongoni mwa wale waliojiandikisha, lakini hawakupiga kura mwaka wa 2020, kwa mujibu wa kura ya maoni ya New York Times/Siena.

Tano, Kamala, amechangisha fedha nyingi na kugharamika zaidi. Sio siri kuwa chaguzi za Mareknai ni ghali na 2024 ni ghali zaidi kuwahi kutokea.

Lakini linapokuja suala la matumizi ya mamlaka Kamala, yuko juu. Amepiga hatua zaidi zaidi tangu kuwa mgombea mnamo Julai akilinganishwa na Trump katika kipindi chote tangu Januari 2023, kwa mujibu wa uchambuzi wa hivi karibuni wa Financial Times, ambao pia ulibaini kuwa kampeni yake imegharimu karibu mara mbili zaidi ya gharama za matangazo.

### CHAGUZI ZILIZOPITA

Uchaguzi wa mwaka 2020, ulifanyika Jumanne Novemba 3. Lakini Televisheni za Marekani hazikumtangaza Joe Biden kuwa mshindi hadi Jumamosi asubuhi ya Novemba 7, baada ya matokeo ya Pennsylvania kuwa wazi zaidi.

Mwaka 2016, Trump aliposhinda urais, alitangazwa mshindi siku moja baada ya uchaguzi. Mwaka 2012, wakati Barack Obama aliposhinda muhula wa pili, ushindi wake ulionekana kabla ya saa sita usiku siku yenyewe ya kupiga kura.

Uchaguzi wa 2000 kati ya George W Bush na Al Gore, ulikuwa tofauti. Kura zilipigwa Novemba, 7. Lakini kulikuwa na mchuano mkali huko Florida na kinyang'anyiro hicho hakikuamuliwa hadi Desemba 12.

Mahakama ya Juu ya Marekani, ilipiga kura kusitisha mchakato wa kuhesabu kura upya kwa jimbo hilo, na Bush akawa mshindi na kumkabidhi White House.

### MAJIMBO GANI MUHIMU 2024?

Kote Marekani, vituo vya kwanza vya kupigia kura vitafungwa saa 23:00 GMT siku ya Jumanne na vituo vya mwisho vitafungwa saa 06:00 GMT, siku ya Jumatano.

Kinyang'anyiro hiki kinatarajiwa kupata matokeo kutoka katika majimbo saba. Majimbo yenyewe ni Arizona, Georgia, Michigan, Nevada, North Carolina, Pennsylvania na Wisconsin.

### KURA HUHESABIWAJE?

Utaratibu wa kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Marekani mara nyingine hutangazwa ndani ya saa chache, baada ya vituo kufungwa. Mshindi wa urais huweza kutangazwa usiku wa siku ya uchaguzi au mapema asubuhi iliyofuata.

Rais mteule ataanza muhula wake wa uongozi, baada ya kuapishwa Jumatatu, Januari 20 mwaka 2025, katika uwanja wa majengo ya Capitol ya Marekani.

Itakuwa ni mara ya 60 kuapishwa kwa rais katika historia ya Marekani. **CHANZO: BBC/DW**

# MEDO APATA MWANGA PA KUANZIA KAGERA SUGAR FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Melis Medo, amesema ushindi wa mabao 2-1 walioupata dhidi ya Dodoma Jiji FC juzi katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, utawarudisha wachezaji wake kisaikolojia na kueleweza matumaini yake kuwa baada ya hapo watafanya vema michezo ijayo.

Huo ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa kocha huyo aliyechukuliwa kutoka Mtibwa Sugar, baada ya kutimuliwa kwa Mganda Paul Nkata, lakini ukiwa wa kwanza kwa Kagera Sugar baada ya michezo minne kupita.

"Ulikuwa ni ushindi muhimu kwetu, niliwakuta wachezaji wakiwa hawako vizuri kisaikolojia, kazi ya kwanza ilikuwa ni kuwatuliza kwani walionekana kama wameanza kukata tamaa, ushindi huu umewafurahisha na inaonekana kabisa wameanza kukaa vizuri kisaikolojia na kuwarudishia ari ya kujituma. Nadhani huu ni mwanzo mzuri kwani watajiona wanaweza na watajituma mara mbili zaidi katika mchezo ujao," alisema kocha huyo.

Mara ya mwisho Kagera Sugar kushinda ilikuwa Septemba 20, mwaka huu ilipoifunga KenGold mabao 2-0, baada ya hapo ilichapwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars, bao 1-0 dhidi ya KMC, na idadi kama hiyo dhidi ya Coastal Union, ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Pamba Jiji. Inashika nafasi ya 14 kwenye msimamo ikiwa na pointi nane kwa michezo 10 iliyocheza.

**Naye Mecky Mexime, amesema wamepoteza mchezo huo kwa sababu wachezaji wake hawakuwa makini dakika 20 za mwanzo.**

"Dakika 20 za mwanzo hatukuwa makini, wakapata mabao mawili ya haraka haraka, tuliporuhusu mabao hayo tulitoka mchezoni kabisa, baadaye wachezaji wangu walitulia na kupata bao moja.

"Ingawa tulipachika bao lililokataliwa, lakini sina uhakika kama lilikuwa halali au la, ila tumepoteza mchezo tunashukuru kwa yote," alisema Mexime.

Mabao katika mchezo huo yaliwekwa wavuni na Pater Lwasa dakika ya 19, na Khasim Fekha dakika ya 23, huku Zidane Sereri akifunga bao la kufutia machozi kwa upande wa Dodoma Jiji.

Timu hiyo ni ya tisa kwenye msimamo ikiwa na pointi 13 kwa michezo 11 iliyocheza mpaka sasa.

## NGOMA...



Kikundi cha Ngoma za Asili cha Makumbusho Dancing Troupe, kikitumbuiza na kucheza pamoja na raia wa kigeni wakati wa mkutano kati ya Wizara ya Maliasili na Utali na China, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi, ukiwa na lengo la kujenga na kuimarisha utalii na utamaduni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Singida BS hawatanii Ligi Kuu Bara*

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Singida Black Stars malengo yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri msimu huu kwa kushika nafasi za juu na wanachokifanya sasa kwenye ligi wamedhamiria, imeelezwa.

Singida Black Stars inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kufikisha pointi 23 kutokana na michezo 10 iliyocheza ambapo inazidiwa pointi moja na vinara wa ligi hiyo, Yanga na ikiizidi Simba iliyopo nafasi ya tatu kwa pointi moja.

Akizungumza na Nipashe jana, msemaji wa klabu hiyo, Hussein Masanza, alisema mipango yao msimu huu ipo pale pale kwa kuleta ushindani wa kweli kwa timu zilizozoea kumaliza katika nafasi za juu.

"Timu yetu itaendelea kupambana katika michezo yote, tumeanza vizuri msimu huu na tunataka kuendelea kufanya vizuri, tuna kila sababu ya kufanya vizuri kutokana na usajili wetu na maandalizi tuliyoyafanya kabla ya kuanza kwa msimu," alisema Masanza.

Alisema anafahamu kila muda unavyozidi kwenda ligi inazidi kuwa ngumu, lakini wamejiandaa kwa ushindani mpaka mechi ya miwsho ya msimu.

"Kila baada ya mchezo mmoja kumalizika kwetu ni maandalizi ya unaofuata, huu msimu ni wetu kwa ajili ya kufanya makubwa kwenye ligi," alisema.

Licha ya Singida kushika nafasi ya pili kwenye msimamo, wanaweza wakaondolewa kwenye nafasi hiyo ikiwa Simba watashinda mchezo wao wa leo dhidi ya KMC.

Simba ikipata ushindi itawashusha Singida Black Stars mpaka nafasi ya tatu kwa kuwa itakuwa imeizidi pointi mbili huku wakiwa na idadi sawa ya michezo.

## Wabunifu mavazi waupamba Usiku wa Shampeni Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WABUNIFU wa mavazi na mitindo wameupamba vilivyo Usiku wa Shampeni katika hafla ya jioni ya kipekee ya sanaa na ubunifu, iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Katika hafla hiyo ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Shampeni, ilipambwa na wabunifu mbalimbali wakiwamo Juma Jux, Ommy Dimpoz, Mtani Bespoke, Kiki Fashion, Branoh Bahati na Victoria Martin.

Wengine ni pamoja na George Williams, Seko Shamte, Grace wa Nyumba ya Kifahari ya Mtindo, Howard, Bianca Mengsen, Pedaah John, Arjun, Mgece na Rio Paul, waungana na Moet & Chandon.

Katika simulizi ya kuvutia kwenye hafla hiyo, Mbunifu na Fundi Cherehani mashuhuri, Mtani Bespoke, alitumia fursa hiyo kuelezea safari yake aliyoifanya Epernay, Ufaransa, katika wasilisho maalum la video iliyonasa matukio muhimu aliyoyafanya yeye na mafundi wengine wa Kiafrika waliokutana kujifunza na kufahamu ubora wa Moet & Chandon.

Aidha, Mtani alitengeneza na kuzindua suti maalum iliyonakshiwa kwa ustadi na urithi wa Tanzania na urithi wa shampeni hiyo, ikijumuisha uwapo wa mashamba ya zabibu kama yale yanayotengeneza shampeni ya Moet and Chandon pamoja na utamaduni wa Kitanzania kupitia urithi wa mavazi ya jamii ya Wamasai.

Janet Mwalilino ambaye ni Mwakilishi wa Chapa ya Moet na Hennesy, alifungua jioni hiyo kwa kusema, "Kaulimbiu ya usiku wa leo, 'Ubunifu Usio na Mwisho katika Ufundi, inaonesha ari yetu ya kuinua nyakati za maisha kwa shampeni na kutumia usanii wetu wa kipekee tulionao.

"Urithi wa Moet & Chandon umejengwa katika kuchanganya mila na uvumbuzi, na tunafurahi kushiriki hili na jumuiya yetu ya Kitanzania".

Mshereheshaji Rio Paul, alisema inatia moyo kuona utamaduni wetu wa Kitanzania ukiheshimiwa kupitia ushirikiano na kinywaji hicho na usiku huo, wanasherehekea talanta na hadithi za kipekee za watu wote waolikuwapo hapo.

Aidha, hafla hiyo, ilihitimishwa kwa onesho la kupendeza na kuvutia la Violin na Agustino, huku wageni wakifurahia kwa pamoja na kubadilishana mawazo kuashiria matukio yao muhimu ya pamoja.

Tukio hili la kukumbukwa lilisisitiza dhamira ya Moet & Chandon katika sanaa, ubunifu kwa kushirikiana na watu wa hapa nchini kuunganisha ushawishi wa Kiafrika na Kifaransa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FERNANDEZ ATAKIWA INTER

INTER Milan na Barcelona zinapanga kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 23, ambaye mustakabali wake Stamford Bridge haujabainika. ***(Sun)***

### ISAK BEI JUU

ARSENAL imemtambua mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25, kama lengo lao kuu la uhamisho, ingawa 'Magpies' wanadai ada ya takriban pauni milioni 100 kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Sweden. ***(Team Talk)***

### UNITED YAMTAKA QUENDA

KLABU ya Manchester United inamtaka winga wa Sporting, Geovany Quenda mwenye umri wa miaka 17, huku mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno chini ya miaka 21, pia akilengwa na Manchester City, Liverpool na Juventus. ***(Team Talk)***

### HAG HAKUMTAKA ZIRKZEE

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Erik ten Hag, hakutaka kumnunua mshambuliaji wa Uholanzi Joshua Zirkzee kutoka Bologna msimu wa joto. ***(Sun)***

### SPURS INAMTAKA REMINDERS

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na kiungo wa kati wa Uholanzi, Tijjani Reijnders mwenye umri wa miaka 26, lakini hawana uwezo wa kumnunua kutoka AC Milan Januari. ***(Football Insider)***

### BADIASHILE HAUZWI

CHELSEA haina nia ya kumuuza mlinzi Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 23, huku beki huyo wa Ufaransa akizingatiwa kuwa sehemu ya mipango yao ya muda mrefu. ***(Fabrizio Romano)***

### TEL HANA MPANGO

KLABU ya Nottingham Forest ingependa kumchukua winga wa Bayern Munich, Mathys Tel mwenye miaka 19 kwa mkopo, lakini mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa wa chini ya miaka 21, hana mpango wa kuondoka Bavaria msimu wa baridi. ***(Sky Germany)***

### LAMPARD ATAJWA ROMA

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Everton, Frank Lampard, ameibuka kama mgombea anayepigiwa upatu kuchukua mikoba ya kocha, Ivan Juric anayekabiliwa na shinikizo ikiwa Roma itaamua kumfuta kazi raia huyo wa Croatia. ***(Gazzetta dello Sport)***

### SON KUZINGATIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur itazingatia chaguo la mwaka mmoja kwenye mkataba wa mshambuliaji wa Korea Kusini, Son Heung-min mwenye umri wa miaka 32. ***(Telegraph)***

### AMORIM KUPEWA RUNGU

MANCHESTER United itampa kocha mpya Ruben Amorim nguvu kabla ya kufanya maamuzi ya mikataba kuhusu wachezaji wanaokaribia mwisho. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# EDU AJIUZULU RASMI ARSENAL

**LONDON,** England

MKURUGENZI wa Michezo wa Arsenal, Edu Gaspar, amejiuzulu wadhifa wake, klabu hiyo ilithibitisha katika taarifa yake jana.

**Edu alijiunga na Arsenal mnamo Julai 2019 kama mkurugenzi wa ufundi na aliongoza mabadiliko ya kitamaduni katika kilabu ambayo yalimwona Mikel Arteta aliyeajiriwa kama kocha na vita vya upande vya kuwania taji la Ligi Kuu katika misimu miwili iliyopita.**

Edu baadaye alipandishwa cheo na kuwa mkurugenzi wa kwanza wa michezo wa klabu hiyo mnamo Novemba 2022.

Muda wa Mbrazil huyo kama mkurugenzi ulikuja baada ya kucheza kwa miaka minne kati ya 2001 na 2005, ambapo alishinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2001-02 na 2003-04 chini ya Kocha Arsene Wenger.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Edu amefuatwa na mmiliki wa Nottingham Forest na mmiliki wa Olympiacos Evangelos Marinakis kuongoza kikundi chao cha klabu na ofa ambayo itajumuisha mshahara ulioongezwa sana.

Vyanzo viliongeza kuwa mazungumzo yako katika hatua ya juu huku Edu akitaka kuchukua nafasi hiyo.

Edu aliwasilisha uamuzi wake kwa maofisa wakuu wa klabu katika uwanja wa mazoezi wa Arsenal wa London Colney Jumatatu asubuhi.

Vyanzo viliiambia ESPN, kuwa kwa sasa haijulikani ikiwa kuna chochote katika masharti ya kuondoka kwake ambayo yatachelewesha kuchukua kazi nyingine.

"Huu ulikuwa uamuzi mgumu sana kufanya," alisema Edu.

"Arsenal imenipa nafasi ya kufanya kazi na watu wengi na nafasi ya kuwa sehemu ya kitu maalum katika historia ya klabu.

"Nimependa kufanya kazi na wenzangu wengi wakuu katika timu zetu za wanaume na wanawake hasa wa Mikel Arteta, ambaye amekuwa rafiki mkubwa.

"Sasa ni wakati wa kutafuta changamoto tofauti. Arsenal daima itabaki moyoni mwangu. Naitakia klabu na mashabiki wake mambo mema tu na kila la kheri."

Mwenyekiti mwenza wa Arsenal, Josh Kroenke, alisema katika taarifa hiyo: "Tunaheshimu uamuzi wa Edu na tunamshukuru kwa mchango wake mkubwa na kujitolea kuisukuma klabu mbele.

"Kila mtu katika klabu anamtakia heri. Sote tunampenda sana na nguvu chanya anayoleta kwa kila kitu na kila mtu.

"Mabadiliko na mageuzi ni sehemu ya klabu yetu. Tunabaki kuzingatia mkakati wetu na kushinda mataji makubwa. Mpango wetu wa urithi utaakisi azma hii inayoendelea."

Kikosi cha Arteta kiko katika nafasi ya tano kwenye ligi, pointi saba nyuma ya vinara Liverpool.

> ●●● Huu ulikuwa uamuzi mgumu sana kufanya, sasa ni wakati wa kutafuta changamoto tofauti...

# NEYMAR APATA MAJANGA TENA




**RIYADH,** Saudi Arabia

NEYMAR aliichezea Al Hilal kwa mara ya pili huku akiendelea kurejea baada ya kutokuwapo kwa mwaka mzima kutokana na kupasuka kwa mfupa wa goti, lakini ameumia tena.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil aliingia uwanjani dakika ya 58 katika ushindi wa mabao 3-0 wa timu yake katika mechi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia Jumatatu, lakini alitolewa chini ya dakika 30 baadaye baada kuumia mguu wa kulia.

Aleksandar Mitrovic alifunga hat-trick na kuiongoza Al Hilal kushinda na kuwaweka kileleni mwa jedwali la Ligi ya Mabingwa Asia.

Neymar aliona mechi yake ya kwanza kwa Al Hilal, ambayo alijiunga nayo 2023 kutoka Paris Saint-Germain, Oktoba 21, lakini hakuwa amecheza tena hadi mechi ya Jumatano dhidi ya Esteghlal kwa vile hawezi kusajiliwa kwa mechi za Saudi Pro League hadi Januari.

Al Hilal walikuwa wamepanga kurejea polepole kwa mfungaji bora wa muda wote wa Brazil, ambaye alipata jeraha la goti wakati wa mechi ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Uruguay muda mfupi baada ya kujiunga na timu ya Saudia na kufanyiwa upasuaji Novemba mwaka jana.

Neymar pia aliachwa kwenye kikosi cha Brazil kwa mechi mbili za kufuzu Kombe la Dunia la Novemba, huku kocha Dorival akisema timu na shirikisho hazitaki kuharakisha kurejea kwake katika timu ya taifa.

Brazil iko nafasi ya nne katika kundi lao la kufuzu Kombe la Dunia, pointi nne nyuma ya vinara Argentina baada ya michezo 10.

# Balotelli ni yuleyule tu

**ROME,** Italia

MARIO Balotelli alicheza mechi yake ya kwanza ya Serie A katika kipindi cha miaka minne alipoingia kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa bao 1-0 wa timu yake ya Genoa dhidi ya Parma Jumatatu, lakini alioneshwa kadi ya njano ndani ya dakika tano tu.

Balotelli aliingia uwanjani dakika ya 86 na alipewa kadi katika dakika za majeruhi baada ya kufanya madhambi.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Italia alisajiliwa na Genoa iliyo hatarini kushuka daraja wiki iliyopita, baada ya kucheza mara ya mwisho kwenye ligi hiyo akiwa na Brescia msimu wa 2019-2020.


Sare ya bila ushindi ya Parma ilifikia mechi tisa na kupoteza, ingawa mwenyeji alipata matokeo bora zaidi kipindi cha kwanza, Valentin Mihaila na Anas Haj Mohamed wakikaribia kufunga bao.

Lakini Genoa walichukua udhibiti baada ya mapumziko, kwani bao la Morten Thorsby lilikataliwa baada ya dakika 49 na Andrea Pinamonti kugonga nguzo muda mfupi baadaye.

Pinamonti alifunga bao la ushindi zikiwa zimesalia dakika 11 alipouwahi mpira uliorudi uwanjani baada ya shuti hafifu la Jeff Ekhator kugonga mwamba.

Ulikuwa ushindi wa kwanza kwa Genoa tangu ilipoilaza Monza mnamo Agosti 24 na kujiongeza kutoka mkiani mwa msimamo na hadi nafasi ya 17. Parma ni ya 15.



# Ancelotti: Soka lilipaswa kusimamishwa Hispania

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema soka lote nchini Hispania lilipaswa kusitishwa baada ya mafuriko huko Valencia na kusababisha vifo vya takriban watu 217.

Mchezo wa Madrid wa LaLiga huko Valencia - ambao ulipaswa kuchezwa Jumamosi - uliahirishwa, pamoja na mchezo wa Villarreal dhidi ya Rayo Vallecano, lakini mechi nane zilizosalia za Ligi Kuu ziliendelea.

LaLiga imekuwa ikishirikiana na Shirika la Msalaba Mwekundu kuchangisha fedha kwa walioathiriwa na mafuriko, baada ya maelfu ya nyumba na biashara kuharibiwa, na viunga vya usafiri kuharibika, katika moja ya majanga makubwa zaidi ya asili katika historia ya hivi karibuni ya Hispania.

"Imekuwa wiki ya msiba, na tuna huzuni," alisema Ancelotti katika mkutano na waandishi wa habari Jumatatu.

"Tuko karibu sana na Valencia na miji yote iliyoathiriwa. Tunatumaini inaweza kutatuliwa hivi karibuni. Kuzungumza kuhusu soka ni vigumu, na pia kucheza soka. Sisi ni sehemu ya nchi hii, na inatuathiri sana."

Madrid, ambao mechi yao ya mwisho walichapwa mabao 4-0 na Barcelona Oktoba 26 jana Jumanne walikuwa wenyeji wa AC Milan katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kichwa chako hakiko katika kazi yako," alisema Ancelotti, alipoulizwa ikiwa imekuwa vigumu kujiandaa.

"Tutajiandaa kwa ajili ya mchezo, kwa sababu sisi ni wataalamu. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya."

HABARI MICHEZO

## Gamondi aanika gonjwa la Yanga

INATOKA UK. 24

hizi za timu, hatuwezi kubadilisha aina ya uchezaji wetu wakushambulia na soka la kasi," alisema Gamondi.

Akizungumzia mchezo ujao wa Ligi Kuu, alisema wamejiandaa vizuri na amehakikishiwa na wachezaji wake kuendelea kupambana kuhakikisha wanapata ushindi kwenye michezo ijayo.

"Ni lazima tusahau matokeo ya mchezo uliopita, nimezungumza na wachezaji wangu na wapo katika hali nzuri, wana hamasa kubwa, kitu kinachoniaminisha tutarejea kwenye fomu yetu ya ushindi," alisema Gamondi.

Mechi ijao Yanga itaikaribisha Tabora United kwenye Uwanja wa Azam Complex kesho, huo ukiwa ni mchezo wa kwanza tangu watoke kupoteza dhidi ya Azam FC kwa bao 1-0 katika dimba hilo.

## Simba yapania kukaa kileleni

INATOKA UK. 24

yake watabadilika kwenye mfumo.

"Hii ni mechi ya nyumbani, hatuwezi kucheza kama zile za ugenini, kocha ametuelekeza jinsi gani ya kucheza mechi za ugenini hasa kwenye viwanja vya mikoani na tukiwa nyumbani kwenye kiwanja bora tucheze vipi," alisema mchezaji huyo ambaye Simba ilimsajili mwanzoni mwa msimu kutokea timu hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moalin, amesema wanatakiwa kucheza kwa umakini na maelewano kwani wanacheza na timu kubwa inayoweza kutumia makosa ya wapinzani kuwaadhibu.

"Mechi itakuwa ngumu, Simba ni timu kubwa, tunatakiwa tucheze kwa umakini na kwa maelewano ya hali ya juu, tunajua tuna mapungufu sehemu ambayo siwezi kuyataja.

Mimi napenda kucheza mpira, napenda wachezaji wangu wainjoi na hiyo ndiyo falsafa ya KMC, nafikiri yeyote atakayefanya makosa mengi ndiye atakayeadhibiwa," alisema kocha huyo.

KMC ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 14 na katika mchezo huo inakwenda kucheza mechi ya 11, huku Simba ikifikisha mechi ya 10.

# AZAM KUSHEREHEKEA USHINDI DHIDI YA YANGA MWEZI MZIMA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC, imesema inaendelea kusherehekea ushindi wao wa bao 1-0 ilioupata Jumamosi iliyopita dhidi ya Yanga na itafanya hivyo hadi Novemba 23, mwaka huu, itakapocheza mechi yake nyingine ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Hasheem Ibwe, jana alisema kwa bahati nzuri baada ya kuwafunga Yanga hawana mchezo mwingine wowote hadi Novemba 23 itakapocheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, hivyo wataendelea kuutumia muda huo kuendelea kusherehekea ushindi huo.

**Aliwataka wanaowabeza kuendelea kushangilia ushindi huo wawaache kwani wanafanya hivyo si kwa sababu wameifunga Yanga, bali pia wamechukua pointi tatu kwa timu wanayogombea nayo ubingwa, vile vile kuwalipia kisasi wote ambao walifungwa na timu hiyo.**

"Sherehe zetu bado zinaendelea tangu Jumamosi tumeendelea kufurahia ushindi dhidi ya Yanga, hakuna wa kutupangia ziendelee hadi lini, vibonzo na utani kwenye mitandao ya kijamii vitaendelea kuwapo, wasituchoke, hayo maumivu wanayopata ndiyo ambayo huwa wanayapata wenzao wanapowafunga.

"Tunafanya hivi kwa sababu si tu kwamba tumeifunga Yanga, lakini tumewafunga Mabingwa Watetezi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, tumeifunga timu ambayo inausaka ubingwa, ukiwa unatafuta ufalme wa soka lazima umfunge yule mnaousaka naye, unakuwa umeshampunguza nguvu na wewe umechukua pointi tatu kutoka kwake.

"Pili Yanga ndiyo mtemi wa wengine, amezifunga timu nyingi tena kubwa, halafu ni timu ambayo ilikuwa haijapoteza mchezo wowote na haijaruhusu bao, yote hayo sisi tumetibua rekodi, kwa nini tusisherehekee wiki nzima? Alitamba Ibwe.

Alisema sherehe hizo zitaendelea hadi Novemba 23, huku wakiwa wamewapa mapumziko wachezaji wao, lakini watarejea tena kwa ajili ya kuanza mazoezi kujiandaa na michezo miwili ya Novemba.

"Baada mechi dhidi ya Yanga, tuna michezo miwili mwezi huu, Novemba 23 dhidi ya Kagera Sugar na Novemba 27 dhidi ya Singida Black Stars, ni michezo migumu, lakini wachezaji wetu kwa sasa wana ari ya ushindi," alisema.

Azam iliyokuwa mgeni kwenye Uwanja wao wa Azam Complex kikanuni, ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Yanga, lililowekwa wavuni na Gibiril Sillah na kuifanya kufikisha pointi 21 kwa michezo 10 iliyocheza ikiwa kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu.

SOKA ZAIDI...



Vijana wakicheza mpira katika Uwanja wa Mchanga wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mwembe Makumbi City yatakata Ligi Kuu Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

PAMOJA na ugeni wao kwenye Ligi Kuu Zanzibar timu ya Mwembe Makumbi City, imerejea katika kasi yake ya ushindi baada ya juzi kuibuka na ushindi.

Mwembe Makumbi City, ambayo huu ni msimu wake wa kwanza kucheza Ligi Kuu Zanzibar, juzi Jumatatu ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Chipukizi FC, mchezo huo ukichezwa katika Dimba la Mau ze Dong majira ya saa kumi alasiri na kujaza mashabiki wao wengi waliombatana na kikundi kilichokuwa kikitoa burudani ya ngoma.

Kwa ushindi huo sasa Mwembe Makumbi City wamerejea katika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu baada ya kufikisha pointi 19.

Nafasi ya tatu inashikiliwa na Mlandege FC yenye pointi 17 huku kinara wa ligi hiyo Mafunzo FC ikiwa na alama 20.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha wa Mwembe Makumbi City, Rajab Mrisho Rajab, alisema kufanya vizuri kwa timu hiyo kunatokana na hamasa kubwa waliyonayo wachezaji wake.

Alisema licha ya kupoteza mchezo wao uliopita, lakini wachezaji walicheza kwa ari na hamasa kubwa ya kupata matokeo. Rajab alisema katika mchezo wa juzi dhidi ya Chipukizi FC, ulikuwa mgumu licha ya kufanikiwa kukata kiu yao kwa kupata pointi hizo tatu.

Alisema wapinzani wao walikuja na mpango wao wa kupata matokeo chanya baada ya kupoteza mchezo wao wa nane, lakini pia na wao walikuwa na malengo kama yao kutokana na kudondosha pointi zote tatu mechi iliyopita.

"Tumefanikiwa kupata pointi tatu katika mchezo huu mgumu, wachezaji walipambana kuona tunafanikiwa lengo letu, lakini haikuwa kazi rahisi," alisema.

Alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa 10 ambao watashuka uwanjani kesho kuvaana na Junguni FC.

Michezo
Jumatano Novemba 6, 2024
Nipashe




Neymar apata majanga tena

UKURASA 22

# Simba yapania kukaa kileleni leo

## ●●● Fadlu aichambua KMC, awageukia mabeki, Awesu naye atema 'nyongo'...

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wowote itakaoupata timu ya Simba leo dhidi ya KMC, utaipeleka kileleni kwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku Kocha Mkuu Fadlu Davids, akionesha furaha kwa kurejea kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

**Simba yenye pointi 22, ikiwa nafasi ya tatu ya msimamo, itafikisha pointi 25 kama ikipata ushindi leo na kuishusha Yanga inayoongoza kwa pointi 24, ambayo nayo itasubiri mchezo wake wa kesho dhidi ya Tabora United.**

Kocha huyo jana alisema kuwa amefurahi mno kurejea tena hapo kwani ni uwanja wao wa nyumbani, lakini unawaruhusu kucheza aina yoyote ya soka wanalotaka.



Simba inarejea kwenye uwanja huo baada ya kupata tabu Ijumaa iliyopita ikicheza ugenini, Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma na kushinda kwa mbinde bao 1-0 dhidi ya Mashujaa FC, ikilazimika kusubiri hadi dakika ya mwisho ya majeruhi kwa bao la Mganda Steven Mukwala.

Pamoja na mambo mengine kocha huyo alilalamikia pia uwanja kuwa haukuwa rafiki kwa wachezaji wake.

"Matayarisho yamekwenda vizuri, najua mechi itakuwa ya ngumu sana, lakini nimefurahi kurejea kwenye dimba la KMC, uwanja ambao tumeuzoea, tunautumia kama wa nyumbani ambao unaruhusu kucheza soka la aina yoyote tunalotaka," alisema kocha huyo.

Simba inatumia Uwanja wa KMC Complex kama wake wa nyumbani, pia kesho kikanuni itakuwa mwenyeji, lakini uwanja huo ni mali ya Manispaa ya Kinondoni inayoimiliki timu ya KMC.

"Kila mechi iko tofauti na mahitaji yake ni tofauti pia, najua watakuja kwa nguvu kwa ajili ya kutukabili, nimeisoma KMC jinsi gani inavyocheza, wanacheza soka la kushambulia moja kwa moja, hivyo itabidi safu yangu ya ulinzi kuwa makini, hebu tuangalie watakavyoanza ili tujue tukabiliane nao vipi," alisema.

Kiungo mshambuliaji wa Simba, Awesu Awesu anayerejea nyumbani KMC, kucheza na timu yake ya zamani, alisema hawawezi kucheza kama walivyocheza dhidi ya Mashujaa FC, badala

INAENDELEA UKURASA 23



Awesu

# Gamondi aanika gonjwa la Yanga

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Miguel Gamondi, amesema kwa sasa timu nyingi zinapokutana na Yanga zinacheza mtindo wa 'kupaki basi' (kukaba wakati wote), na kwamba hicho ndicho kinachosababisha kushindwa kucheza soka lao walilolizoea, kitu ambacho anakichukia.

Gamondi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa kwake yeye mfumo wake ni kushambulia na kucheza mpira wa kasi, lakini changamoto ni kucheza na timu inayokaa golini kuzuia tu.

"Tumekuwa tukikamiwa sana, napenda kucheza mpira, tuoneshane ufundi na mbinu, lakini tunashindwa pale tunapokutana na timu ambazo wao wanawaza kukaa wengi kwenye eneo lao (kupaki basi)," alisema Gamondi.

Aidha, alisema tayari ameanza kufanyia kazi mbinu zitakazowasaidia kupata ushindi mzuri wanapokutana na aina ya timu hizo zinazopaki basi.

"Tunafanyia kazi mbinu za kuhakikisha tunacheza soka letu tunapokutana na aina




INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >